# Nipashe

Jumanne Juni 28, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580990 *

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



SportPesa

JACKPOT BABA LAO!

TZS. 267,714,020

CHEZA SASA KWA 1000/= TU!

SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#




## JK aona nuru Taasisi ya Ruge Mutahaba

UKURASA 4




## WAKALA AKANUSHA MANE KULIPWA KIDOGO LIVER

UKURASA 22

## YALIYOMO


UKURASA WA 3

**6 WAFARIKI DUNIA AJALI LORI, WAMO ASKARI JWTZ**

WATU sita wakiwamo askari watatu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ)...

UKURASA WA 5

**CHADEMA YATAKA ZUIO LA MIKUTANO YA SIASA LIFUTWE**

MKUTANO wa Kanda ya Ziwa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA)...

UKURASA WA 19

**MWALIMU ALIYEJIFUNGUA PACHA WANNE KUPEWA HUDUMA MAALUM**

MKUU wa Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma, Julius Mtatiro, amemtaka...




Mwalimu Judith Abiudi Sichalwe (kushoto), aliyejifungua watoto wanne akiwa pamoja na Mkuu wa Wilaya ya Tunduru, Julius Mtatiro (watatu kushoto), alipomtembelea nyumbani kwake katika kijiji cha Mkapunda Wilaya ya Nalasi juzi. Wapili kulia ni mume wake, Hamisi Shaibu. **PICHA: STEVINE CHINDIYE**

## Rais Samia afichua siri safari kisiasa

UKURASA 3

# KILIO TOZO MIAMALA CHASIKIKA

UKURASA 2

Tozo zilizopunguzwa



~~Sh.10,000~~

**Sh. 4,000**

Tozo miamala ya simu kutoa Sh. 10,000 hadi Sh. 4,000



~~Sh.3,000~~

**Sh. 500 -2,000**

King'amuzi kimepunguzwa tozo kutoka kiasi cha Sh. 3,000 hadi Sh. 500 - 2,000

Tozo zilizoongezwa




-Bidhaa kutoka nje, pipi, chokoleti-Sh.700 hadi 1,000

-Chuma chakavu (kwenda nje)- Tani moja Sh. 138,000

Tozo zinazopendekezwa

- Magari ya kigeni (yanayopita nchini)
  - Sh. 23,240 kwa kilometa 100
- Uchafuzi mazingira- Sh. 139,441
- Malori- Sh.232,401 (yanapovuka mpaka)



Picha; mtandao, ubunifu; Kondo Harun. binharun79@gmail.com

# ACT-Wazalendo yataja maeneo 8 kuboreshwa

UKURASA 2


MICHEZO **SIRI UBINGWA YANGA SC HII** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6




Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, akiwasisitiza wabunge wa Baraza la Wawakilishi (hawapo pichani), kuchangamkia fursa mbalimbali za uwekezaji zitolewazo na Benki ya CRDB wakati wa semina maalumu iliyotolewa na benki hiyo mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Hamad Hassan Chande na katikati ni Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (aliyetoa mada katika semina hiyo), jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yakubali kupunguza tozo miamala simu, ving'amuzi

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

SERIKALI imekubali kupunguza tozo ya miamala ya simu na ving'amuzi baada ya kufanyika kwa majadiliano na Kamati ya Bunge ya Bajeti.

Katika punguzo hilo, tozo ya ving'amuzi imeshuka kutoka Sh. 3,000 hadi kiwango cha Sh. 500 mpaka 2,000, huku tozo ya miamala ya simu ikishuka kutoka Sh. 10,000 hadi 4,000 na kuondoa sharti la lazima kwa kila Mtanzania mwenye umri wa miaka 18 akinunua au kuuza bidhaa awe na namba ya mlipa kodi (TIN).

Akiwasilisha maoni ya Kamati ya Bajeti, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Sillo Baran, wakati wa mjadala wa Muswada wa Sheria ya Fedha 2022, alisema serikali ilileta pendekezo la kuanzisha tozo ya Sh. 1,000 hadi Sh. 3,000 kwa ving'amuzi itakayokuwa ikitozwa kupitia malipo ya vifurushi.

Baran ambaye ni Mbunge wa Mbulu Vijijini alisema serikali pia imekubali kusitisha utozaji wa Sh. 20 kama kodi ya awali kwenye mafuta ya petroli na dizeli wauzaji wa jumla wanapowauzia wafanyabiashara wa rejareja.

Alisema suala hilo lilionekana kuleta mtafaruku katika sekta ya uuzaji wa mafuta nchini pamoja na kuongeza gharama za uendeshaji.

"Kamati ilikubaliana na serikali kupanua mawanda ya utozaji wa tozo hii kwa miamala yote ya kielektroniki. Hivi sasa kuna baadhi ya miamala ilikuwa haitozwi na hivyo kukwepa tozo hii. Hatua hii haitahusisha uhamishaji wa mishahara kutoka benki moja kwenda nyingine," alisema.

**KODI MIAKA 18**

Baran alisema baada ya majadiliano ya kina kamati iliishauri serikali kukubali kuondoa sharti la lazima la mtu popote atakapokuwa anafanya ununuzi au kuuza bidhaa lazima awasilishe namba ya mlipa kodi kwa sababu jambo hilo haliwezekani kwa mazingira nchi.

Alisema pia kuacha mamlaka ya kusamehe riba na adhabu kwa Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kama ilivyo sasa na kuyatambua maghala yaliyoanzishwa kwa misingi ya biashara, isihusu maghala pamoja na vihenge ambavyo vinatumika na wakulima kuhifadhi mazao yao.

"Nipende kulihakikishia Bunge lako tukufu habari potofu za kwamba eti serikali imekusudia kutoza kodi kwa kila mtu aliyefikisha umri wa miaka 18 sio za kweli.

"Lengo ni kuwatambua wananchi wote katika mfumo wa kodi ili pindi wapatapo ajira ama kuanzisha biashara wasipate tabu ya kutafuta Namba ya Mlipa Kodi (TIN) na badala yake iwe ni kuziuhisha tu," alisema Baran.

**SERIKALI KUKOPA**

Baran alisema baada ya majadiliano ya kina na serikali, Kamati ya Bajeti ilikubaliana na ongezeko la serikali kukopa kutoka Benki Kuu ya Tanzania (BoT), kiwango hicho kikokotolewe kutokana na mapato halisi ya mwaka wa fedha uliopita na sio mwaka wa fedha unaotekelezwa.

Alisema hatua hiyo itaepusha kuwa na mzigo wa deni kubwa endapo mapato ya bajeti ya mwaka inayotekelezwa hayatafikiwa kwa asilimia 100.

Alisema mabadiliko yanayofanywa kwenye sheria ni kuongeza wigo wa serikali kukopa kutoka BoT kwa wastani wa asilimia 12.5 wa makusanyo halisi ya mwaka wa fedha uliotangulia na kuwa asilimia 18 ya makusanyo yanayokadiriwa katika mwaka wa fedha unaotekelezwa.

**BIDHAA ZENYE MADHARA**

Alisema serikali inatarajia kuanzisha ushuru wa bidhaa kwa lengo la kudhibiti madhara na kiafya yanayoweza kujitokeza kutokana na matumizi yake.

Baran alisema: "Kamati inapendekeza kutokutoza ushuru kwa bidhaa hizo zinazozalishwa nchini ambazo zimetajwa ikiwamo pipi na chokoleti zinazozalishwa na viwanda vya ndani.

"Kamati imebaini kwamba viwanda hivi vina hali mbaya ya uzalishaji kutokana na kupanda kwa bei za malighafi zinazotumika kuzalisha bidhaa hizi, ndizo biashara kuu ya wafanyabiashara wadogo waliopo katika maeneo ya stendi kuu za mabasi.

"Na nchi jirani katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) hazitozi kodi hii na kwa sababu tuko kwenye jumuiya moja bidhaa hizi kutoka nchi jirani zitakuwa na bei nafuu kuliko zinazozalishwa nchini na hivyo kuleta ushindani usio sawa," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema kamati ilipendekeza kwa serikali kuongeza ushuru wa bidhaa hizo za nje kutoka Sh. 700 iliyopendekezwa hadi 1,000 na kusamehe zinazozalishwa nchini mpaka hali itakavyotengemaa.

"Serikali ilikubali pendekezo la kuongeza bei ya bidhaa hizo kutoka nje hata hivyo haikuondoa ushuru wa bidhaa za ndani," alibainisha.

**CHUMA CHAKAVU**

Alisema Kamati ya Bajeti inakubaliana na mapendekezo ya serikali ya kuanza kutoza asilimia 30 ya FOB "Free on Board" au Dola za Marekani 150 (Sh. 348,602) kwa tani, kwa chuma chakavu kinachosafirishwa nje ya nchi kwa lengo la kuhakikisha viwanda vya ndani vinavyotumia malighafi inapatikana kwa wingi na kwa bei nafuu nchini.

**MAGARI YA KIGENI**

Baran alisema Kamati ya Bajeti ilibaini kuwa licha ya nchi za SADC kukubaliana kutotoza tozo nyingine kwenye magari ya kigeni yanayopita katika nchi husika cha Dola za Marekani 10 (Sh. 23,240) kwa kila kilometa 100, nchi hizo zinatoza tozo nyingine.

Alizitaja tozo hizo kuwa Park Fee (ushuru wa megesho) na kwamba malori ya Tanzania yatatozwa kiasi cha Dola za Marekani 100 kila yaingiapo nchi husika. Alitaja tozo zingine ni ya uchafuzi wa mazingira ambayo hutozwa Dola za Marekani 60 (Sh. 139,441) kwa mwaka na kuna tozo ya ushuru wa vizuizi ya kiasi cha Dola za Marekani 100 (Sh. 232,401) ambayo hutozwa baada ya lori kufika kwenye mpaka wa nchi husika.

"Hatua hii ikichukuliwa inawezekana nchi jirani wasitishe kutoza tozo hizo au kutoza kwa viwango sawa," alisema.

# ACT-Wazalendo yataja maeneo 8 kuboreshwa

**Na Sabato Kasika**

CHAMA cha ACT-Wazalendo, kimempongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa jitihada za kuiletea nchi maendeleo, huku ikiainisha maeneo nane yanayopaswa kufanyiwa maboresho zaidi.

Waziri Kivuli Sekta ya Vijana na Ajira wa chama hicho, Mwalimu Philbert Macheyeki, aliyasema hayo kupitia taarifa yake kwa vyombo vya habari.

Alisema miongoni mwa jitihada zinazofanywa na Rais Samia za kuleta maendeleo ni kutafuta maridhiano ya kitaifa, kuifungua nchi katika sekta ya utalii na uwekezaji na kuimarisha sekta ya kilimo.

Aliyataja maeneo yanayopaswa kuangaliwa kwa jicho la tatu kutokana na uzito wake kuwa ni ukosefu wa ajira kwa vijana.

Aidha, kupanda kwa gharama za maisha ikiwa ni pamoja na kuzuia mfumko wa bei kwenye bidhaa muhimu kama mafuta, sukari, vyakula, utitiri wa tozo na upotevu wa fedha za umma.

"Kutopanda kwa mishahara ya wafanyakazi hususani kwa sekta binafsi, mfumo wa elimu usiozalisha wataalamu wenye ujuzi na kujitegemea, uchaguzi huru na haki, madai ya katiba mpya na tatizo la utolewaji wa mikopo kwa vijana katika halmashauri," alisema Mwalimu Macheyeki.

Alisema mkazo upo kwenye utitiri wa michango shuleni na uduni wa elimu inayotolewa katika shule za msingi, sekondari na vyuo vikuu.

"Suala la michango shuleni na ubora wa elimu itolewayo katika shule na vyuo vyetu ni jambo tete, ni muhimu kujadiliwa kwa uzito kuliko hata hoja ya elimu bure au elimu bila ada," alisema.

Mwalimu Macheyeki alisema shida ya Watanzania wengi sio elimu bure kwa kuondoa Sh. 20,000 au 70,000 zilizokuwa zinatolewa na wazazi/walezi kama ada, bali ni ubora wa elimu.

Alifafanua kwa sasa michango inayochangishwa katika shule za msingi na sekondari ni zaidi ya mara 20 ya kiwango cha ada kilichoondolewa, hali ambayo amedai inachangia kuwaumiza wazazi na walezi.

"Serikali ichukue dhamana ya ubora wa elimu na michango yote na sisi wazazi iturudishie ada na kazi iendelee. Kiwango cha michango inayochangishwa kwa sasa shuleni hususani shule za umma ni kikubwa," alisema.

Pia, alisema kiwango hicho kinakatisha tamaa wazazi na kurudisha nyuma jitihada na maana nzima ya serikali katika kutoa elimu bure ikilinganishwa na ubovu wa miundombinu na ubora wa elimu inayotolewa katika shule hizo.

Mwalimu Macheyeki alisema elimu bora ni muhimu zaidi kuliko elimu bure na jamii inaweza kupimwa kwa kuangalia uwezo, ujuzi, weledi na maarifa kwa wahitimu wa sekondari na vyuo.

Alitaja sababu zinazochangia wahitimu nchini kukosa ubora ni kushindwa kubadili mifumo na mitaala ya elimu, kutoruhusu ushindani huru wa ubora katika utoaji wa elimu kati ya taasisi za umma na binafsi na mazingira mabovu ya kujifunzia na kufundishia hasa kwa shule na vyuo vya umma.

## 6 wafariki dunia ajali ya lori, wamo askari JWTZ

**Halima Ikunji,** TABORA

WATU sita wakiwamo askari watatu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), wamepoteza maisha baada ya gari binafsi walilokuwa wakisafiria aina ya Toyota Mac X kugongwa na lori aina ya Scania kwenye kona.

Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Tabora, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP), Richard Abwao, amethibitisha kutokea ajali hiyo.

Alisema ajali hiyo ilitokea juzi majira ya saa 6.30 mchana katika kijiji cha Inala nje kidogo ya Manispaa Tabora, Barabara ya Itigi.

Abwao, alisema ilisababisha vifo vya askari hao na ndugu zao wengine watatu waliokuwamo katika gari hilo aina ya Toyota Mac X lenye namba T 727 DNX lililogongwa na lori aina ya Scania lenye namba T 557 DNZ.

Alitaja majina ya askari waliopoteza maisha kuwa ni Sixmund Patrick (33), Seleman Omari Pandu (22) na Simai Hamis Simai (35), wote wakazi wa Manispaa ya Tabora.

Aliwataja raia waliofarika katika ajali hiyo kuwa ni Maulid Seleman Maulid (22) na Yusuph Maulid Masegenya (43) wakazi wa Dar es Salaam na Maulid Hussein (28), mkazi wa Tabora.

Alisema chanzo cha ajali hiyo ni mwendokasi na kutokuwa makini barabarani dereva wa gari dogo lililokuwa na askari hao, ambaye alijaribu kulipita lori kwenye kona na kusababisha wagongwe na kupoteza maisha.

Akizungumzia ajali hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dk. Batilda Burian, aliwataka askari wa kikosi cha usalama barabarani kudhibiti mwendo kasi wa vyombo vya moto.

Aliwataka wasimamizi wa vizuizi vya mapato vilivyoko katika maeneo mbalimbali kuviwekea alama zinazoonekana wazi magari yote kwa kuwa vimekuwa vikisababisha ajali.

Aidha, aliagiza wakuu wa wilaya na wakurugenzi wa halmashauri zote mkoani humo kulifanyia kazi suala hilo kwa kuhakikisha vizuizi vilivyoko katika maeneo yao vinatumika vizuri ili kuepusha ajali.

Dk. Batilda alisema miili ya askari waliopoteza maisha imesafirishwa kwa helikopta kwenda nyumbani kwao Zanzibar na Njombe kwa ajili ya maziko huku miili ya raia watatu ikitarajiwa kuzikwa mkoani humo.



Rais Samia Suluhu Hassan akiangalia kazi mbalimbali za kijasiriamali zinazofanywa na wanufaika wa Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote (EOTF) katika maadhimisho ya kilele cha mfuko huo yaliyofanyika ukumbi wa Mikutano wa Julius Nyerere JNICC jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Rais Samia afichua siri safari ya kisiasa

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan, jana amefichua siri ya safari yake ya kuwa mwanasiasa kwa kumtaja Mwenyekiti na Mwasisi wa Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote (EOTF), Mama Anna Mkapa kuwa ndiye aliyemwongoza njia.

Aidha, alisema yeye ni mmoja wa wanufaika wa mfuko huo, ulioanzishwa miaka 25 iliyopita na mke wa Rais wa Serikali ya Awamu ya Tatu.

Alitoa ushuhuda huo, jijini Dar es Salaam alipokuwa mgeni rasmi katika hafla ya maadhimisho ya miaka 25 ya mfuko huo na kutoboa siri ya maneno aliyoambiwa na Mama Mkapa, kuhusu uwezo wake wa kuwa mwanasiasa na yalimpa nguvu ya kujitosa katika tasnia hiyo.

Akisimulia safari yake, alisema siku moja alipokuwa kwenye shughuli moja ya EOTF, aliachwa na gari alilokwenda nalo, Mama Mkapa alipomwona amesimama akamwambia aingie kwenye gari lake na wakiwa njiani katika mazungumzo yao ndipo alipomshawishi kuingia katika siasa.

"Lakini nikiwa ndani ya gari lake alikuwa na mazungumzo yafuatayo, akaniambia Samia nimekuona unavyokwenda na unavyofanya, wewe ni mwanasiasa mzuri sana.

"Uchaguzi unaokuja ungejaribu kuingia, nikamwambia mama mimi sijui hata watu wanaingiajie, akaniambia wewe ulizauliza tu huko kwenu Pemba utaingia... basi nikajaribu na safari ikaanza hapo," alisema.

Rais Samia alisema licha ya ushawishi, mfuko huo ulimjengea uwezo hali iliyochangia kumwiimarisha kisiasa hadi kufikia cheo alichonacho sasa.

Alifanunua kuwa maendeleo ya jamii ni moja ya vipaumbele muhimu katika mipango ya serikali ya awamu ya sita na inasimamia kwa ukaribu upatikanaji wa huduma zote za jamii kwa wananchi.

"Nafurahi kuna mlivyojituma katika kuendeleza maisha yenu, kujiendeleza kijamii, kujiendeleza kiuchumi hadi leo mmefika katika hali hii ambayo nimewakuta, lakini kubwa mmeisaidia EOTF kutekeleza sera ya maendeleo ya jamii ya Juni 1996," alisema.

Aliushukuru mfuko huo kwa kuiunga serikali mkono katika nyanja za kiuchumi, afya na elimu na kutoa wito kwa mashirika yasiyo ya kiserikali pamoja na taasisi za kidini kutoa na kuchangia maendeleo ya jamii hasa wanaoishi katika mazingira duni.

Alisisitiza umuhimu wa elimu kuendelea kutolewa kwa jamii hasa wanawake wahamasike na kutotelekeza watoto wao ili kuepuka watoto wa mitaani.

"Tunapowatelekeza na asipotokea mtu wa kuwaokota na kuwaweka pamoja na kuwaendeleza tunazalisha taifa lenye watoto wasiojitambua, wasio na pakushika, mwisho tunazalisha wanaomsumbua mkuu wa mkoa hapa (Amos Makalla) 'panya roads'," alisema.

### LENGO KUANZISHWA MFUKO

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Mfuko huo, Mama Mkapa alisema, ulianzishwa mwaka 1997 kwa lengo la kuiwezesha jamii ya Tanzania kupiga vita umaskini, ujinga na maradhi.

"Jukumu kubwa la taasisi hii ni kuwawezesha na kuwakomboa wanawake na vijana wanaoishi katika mazingira duni kushiriki kikamilifu katika kutambua uwezo wao na kutumia rasilimali zilizoko kujiletea maendeleo yao ya kiuchumi, kielimu na kiafya hivyo kuondoa umaskini Tanzania," alifafanua.

Kadhali, alisema jamii inapaswa kuwajali wanawake na vijana ambao ni asilimia 53 ya Watanzania kwa kuwa bila kufanya hivyo kundi kubwa litakosa mahitaji yao ya msingi kama elimu, huduma za kiafya na fursa za kiuchumi na kuishi katika lindi la umaskini.

Vile vile, Mama Mkapa alisema katika miaka 25, EOTF imewanufaisha jumla ya wanawake wajasiriamali 6000, kuzalisha ajira 23,000 na kuuza bidhaa za Sh. trilioni 11 kupitia mpango wa kupambana na umaskini ambao huwawezesha wanawake na vijana wajasiriamali kujikomboa kiuchumi kupitia mafunzo na maonyesho makubwa ya biashara.

Pia mpango wa pili ni wa elimu ambao Watanzania 1,755 kutoka jamii maskini wamesomeshwa katika shule za awali hadi vyuo vikuu ndani na nje ya nchi pamoja na kuzisaidia shule katika ukarabati, kugawa vitabu, uchimbaji wa visima salama, vyoo, vitimwendo kwa wanafunzi wenye ulemavu na madawati.

Alitaja mradi mwingine kuwa ni wa afya uliolenga mama na mtoto katika elimu ya afya ya uzazi, maradhi kama kansa, malaria, UKIMWI na UVIKO -19. Pia ujenzi wa wodi ya wazazi na watoto, huduma ya kuhifadhi maiti, ujenzi wa zahanati na vifaa mbalimbali vya hospitali.

### WANUFAIKA WAZUNGUMZA

Mmoja wa wanufaika wa mfuko huo, Naibu Mwakilishi wa Kudumu Umoja wa Mataifa Geneva nchini Uswizi, Balozi Hoyce Temu, alisema amekuwa mtoto pekee aliyefika elimu ya chuo kikuu katika familia yake ya watoto saba kutokana na msaada wa huo.

"EOTF imekuwa msaada kwa watoto wa kike bila ya kuangalia umetoka wapi, wanaangalia uwezo wako, mimi nimetoka kwenye familia ya kawaida, baba na mama yangu walikuwa wanafanya kazi polisi na kupitia taasisi hiyo nilifanikiwa kusoma chuo kikuu Marekani masomo ya mawasiliano ya umma na lugha ya Kifaransa," alisema Hoyce.

Alimshukuru mwenyekiti huyo kwa kumkomboa kielimu na kutimiza ndoto yake ya kuendelea na masomo na kuwaomba wadhamini waendelee kuuangalia mfuko huo kwa sababu unafanya mambo makubwa ya kuwainua wanawake.

Naye mmiliki wa GV Furaha inayojishughulisha na uuzaji wa batiki, Violet Mmanyi, alisema kupitia mfuko huo biashara yake imekua kutoka kuuza kitaifa hadi kimataifa.

Alisema kuwa tangu alipojiunga na mfuko huo amepata fursa ya kusafiri nje ya nchi na kutumia banda la EOTF kuuza bidhaa yake jambo lililochangia kutimiza ndoto yake ya kuwa mfanyabiashara mkubwa.

Naye Neema Riziki (13) anayelelewa na mfuko huo kupitia Kituo cha Kulelea Watoto cha Kibaha, alisema mfuko huo unatimiza haki yake ya kupata elimu na sasa anasomeshwa Shule ya Sekondari Jitegemee kidato cha tatu.

Aliwasihi wazazi kushikamana na kutowatelekeza watoto kwa kuwa wanawasababishia madhara ikiwamo kuathirika kisaikolojia.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi (katikati), akishuhudia utiaji saini ujenzi miradi mitatu ya maendeleo baina ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Taasisi ya Misaada ya Sheikh Zayed Al Nahyan kutoka Nchi za Jumuiya ya Falme za Kiarabu (UAE), hafla iliyofanyika Ikulu ya Zanzibar. Kulia ni Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Dk. Juma Malik Akili na Katibu Mkuu wa Jumuiya hiyo, Hamad Bin Kurdous Al-Amry. **PICHA: IKULU**

# JK aona nuru Taasisi ya Ruge Mutahaba

**Na Romana Mallya**

RAIS mstaafu wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete, amesema Ruge Mutahaba alikuwa na maono ambayo yanapaswa kuenziwa kupitia taasisi yake iliyoanzishwa kwa jina la mwasisi huyo wa Clouds Media Group.

Akizungumza juzi katika uzinduzi wa Taasisi ya Ruge Mutahaba uliofanyika mkoani Dar es Salaam, Rais Kikwete alisema katika kipindi kifupi cha uhai wake, Ruge alifanya mambo mengi mazuri ambayo hayana budi kuenziwa, kukumbukwa na kuendelezwa.

Kikwete alisema taasisi hiyo ni chombo na nyenzo mwafaka wa kusaidia maono yake.

"Nilimfahamu kwa karibu Ruge tangu nilipokuwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini, haikuwa rahisi kutokumfahamu Ruge, alikuwa kama taa iliyowashwa na kuwekwa kwenye kiambaza cha nyumba, Ruge aligusa maisha ya wengi, vijana kwa wazee, matajiri kwa maskini, viongozi na wananchi wa kawaida.

"Leo ni siku ya furaha na faraja kuona jitihada alizozifanya wakati wa uhai wake zinakwenda siyo tu kuenziwa, bali kuendelezwa kupitia taasisi hii inayozinduliwa leo (juzi)," Kikwete alipongeza.

Alisema alifanya kazi kwa karibu na Ruge wakati akiwa Rais na hata baada ya kustaafu na kulikumbusha jambo kubwa ambalo kwa mara ya kwanza kufanya naye ni pale alipomwalika kuwa mgeni rasmi wakati wa uzinduzi wa Kituo cha Ubunifu katika sanaa ya muziki 'Tanzania House of Talents (THT).

Alisema hakusita kumkubalia kwa sababu alivutiwa na maono yake na madhumuni ya kuanzishwa kwa kituo hicho chenye lengo la kutoa fursa kwa vijana wenye vipaji vya muziki, kuendelezwa kwa kuwa wengi walikuwa hawavitambui vipaji vyao na hata waliokuwa wanatambua, hawakuwa na uwezo wa kuviendeleza wenyewe.

Alisema kuwa katika shughuli hiyo, Ruge aliiomba serikali isaidie kupata 'Master Studio', ombi ambalo lilijibiwa, uwekezaji huo ukigharimu siyo chini ya Dola za Marekani 75,000.

Pia alisema Novemba 26, mwaka 2013, Ruge alimwalika kushiriki katika warsha ikiyoitwa 'Kamata Fursa, Twenzetu' iliyofanyika jijini Dar es Salaam ambayo ilikutanisha na kuhamasisha vijana kujituma na kufanya kazi ili kutokomeza ukosefu wa ajira na umaskini wa kipato.

Kikwete alisema kuwa mbeba maono huyo alilikumbusha kundi hilo kuwa fursa za kujiletea maendeleo zimejaa tele nchini na siku hiyo baadhi yao walishuhudia namna walivyofanikiwa kwa kujiajiri na kuajiri wengine.

Pia alisema wasanii walishuhudia namna walivyoziona fursa na kuzitumia na wenzao, walivyokua na kupata mafanikio.

"Kijana Ruge alitoa mchango muhimu kwa safari ya wasanii hao mpaka kufikia walipo sasa, alikuwa jasiri kwenye kuonyesha njia, mtu mwenye moyo wa uthubutu na mjasiriamali aliyejali ubora wa kazi azifanyazo, ndiyo maana kila jambo alilolianzisha lilikuwa na mafanikio.

"Hakufikiria tu maslahi yake mwenyewe, alifikiria namna ya kutoa fursa kwa watu wengine, huo ni moyo wa kipekee na adimu katika dunia ya sasa," alisifu.

Kikwete aliwataka waliokabidhiwa taasisi hiyo, wahakikishe inaakisi taswira ya maono na maisha ya Ruge.

"Ninaomba mkumbuke kuwaendeleza vijana wenye vipaji mbalimbali, vijana wabunifu na vijana wenye moyo wa kujituma katika sanaa na muziki, wale wanaotoka katika familia za chini na mazingira magumu wapewe kipaumbele.

"Kwa namna hiyo mtakuwa mmemuenzi Ruge ipasavyo, naye huko aliko atakuwa akitabasamu kila akiangalia namna mbegu aliyoipanda katika jamii ikichipua na kumea kwa namna ambayo yeye mwenyewe angetaka iwe," alisema.

Waziri wa Nishati, Januari Makamba, alisema vijana wengi wamefanikiwa kutokana na ushauri, msukumo, hamasa na mfano wake na yeye akiwa miongoni wa wanufaika.

"Tumekuwa marafiki wa karibu sana, tumeongea vitu vingi, tumefanya vitu vingi pamoja, tumeshauriana mambo mengi, kwa kweli sitakuja kumsahau hata kidogo," alisema. Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, alisema kupitia programu yake ya 'Tunakufungulia Dunia, Kuwa Unavyotaka', mbeba maono huyo aliamini kuna kazi ya kufungua dunia lakini suala la kwenda ni mtu mwenyewe anataka aende mpaka wapi.

Mkurugenzi wa Clouds Media Group, Joseph Kusaga, alisema Ruge alikuwa mdogo wake, rafiki yake na alikutana naye miaka 26 iliyopita, wakati huo Clouds ilikuwa inapiga disko zaidi.

"Wakati ule alikuwa anasoma na kila akija Tanzania alikuja na muziki na wakati ule muziki ulikuwa adimu sana, ni kama mtu analeta dhababu, kwa sababu kulikuwa hakuna njia ya kuununua kama sasa.

"Ni watu ambao tulipambana sana kulia kushoto, vita vingi tulipigwa lakini tulisimama imara kujenga misingi imara ambayo leo ameacha watu wengi wa kuhakikisha gurudumu linasogea mbele," alisema.

Mama wa Ruge, Christiana Mutahaba, alisema siku hiyo ni ya furaha kwa familia ya Profesa Mutahaba, kwa sababu ya kupata nafasi ya kuona upendo walioutoa kwa mtoto wao.

Alisema wanatambua safari ya kuanzishwa kwa taasisi ya Ruge siyo kazi ndogo na kuvishukuru vyombo vya habari, marafiki na wananchi kwa kujitoa ili kufanikisha kutengeneza maandiko ambayo taasisi hiyo itayasimamia.

"Haya maandiko yalitokana na wadau kukaa pamoja na kutafuta wadhamini wa taasisi ambao waliitikia wito chini ya Mwenyekiti wao, Profesa Rwekaza Mukandala (Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi hiyo), hatuna cha kuwalipa tunawaombea kwa Mungu.

"Tunaimani taasisi ipo kwenye mikono salama. Tunaamini tutashirikana kuleta maendeleo na mitazamo chanya katika Taifa letu," alisema.

Prof. Mukandala alisema imepita miaka mitatu tangu Ruge afariki dunia na enzi za uhai wake alikuwa na vipaji vingi, ari ya kujituma, maono na uwezo mkubwa wa kuhakikisha ndoto zinafanikiwa.

"Katika muhktadha huo tumeona ni muhimu familia, wafanyakazi wenzake na ndugu waliofanya naye kazi kushiriki katika miradi mbalimbali aliyoibua na kuisimamia na waliguswa kwa njia moja ama nyingine na maisha yake na kujitolea kwake na mafanikio yake na maono yake kwamba tushirikiane kuanzisha taasisi hii ambayo itahakikisha yote aliyoyafanya hayatasahaukika na urithi aliouacha unaendelea kuenziwa na vijana wenye vipaji watazidi kuibuliwa na kupewa nafasi kubuni mambo na kuendeleza karma zao, kupata ajira na kujiajiri," alisema.

Mjumbe wa Bodi hiyo, John Ulanga, alisema taasisi imelenga kusaidia vijana wa kike na wa kiume kwa kuangalia maeneo makubwa matatu, upatikanaji wa taarifa na maarifa ukilenga kuwafikia vijana 5,000 kwa mwaka.

Eneo la pili ambalo litawafikia vijana 10,000 kwa mwaka alilitaja kuwa ni kutoa elimu, maarifa na uwezeshaji wa kuunganisha sekta mbalimbali ili kufungua fursa za kiuchumi katika kilimo na mitandao na la tatu kutengeneza kituo kitakachokutanisha kundi hilo kujadiliana ambalo kwa mwaka wanatarajia wawe 1,000.

Katika uzinduzi huo, vijana wa THT walimuenzi kwa kuimba nyimbo alizozipenda na kazi mbalimbali ambazo aliziibua na kuzisimamia, wahusika wake wakitoa ushuhuda namna Ruge alivyogusa maisha yao binafsi na kuwaonyesha njia ya kupitia maono waliyokuwa nayo.

# Mwinyi aahidi SMZ ushirikiano Mahakama kikanda

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema kila nchi ina mafanikio na changamoto katika kutekeleza na kulinda haki za binadamu.

Alisema miongoni mwa mambo yanayolalamikiwa ya kudhihirika uvunjwaji wa haki hizo ni pamoja na baadhi ya makundi kunyimwa haki za msingi, uonevu, ukatili, unyanyasaji, kutokuwapo uhuru katika masuala muhimu na ubaguzi wa aina mbalimbali.

Aliyasema hayo mjini hapo, wakati akifungua kongamano la majaji wa mahakama za kikanda lililoandaliwa kwa lengo la kujadili masuala mbalimbali ya kimahakama, kisheria na haki za binadamu barani Afrika.

Alisema mjadala huo utakuwa na tija kubwa na maazimio watakayoyapitisha yatalenga katika kutafuta ufumbuzi wa changamoto hizo kwa lengo la kuimarisha ustawi wa wananchi barani Afrika na duniani.

"Navutiwa kuona kwamba mada mlizozichagua kwa ajili ya majadiliano zimegusa maeneo muhimu kwa maendeleo ya mahakama na demokrasia barani Afrika," alisema.

Alisema Serikali ya Zanzibar imenufaika kutokana na uamuzi wa kufanyika kwa kongamano hilo ambalo limetoa nafasi kwa majaji na viongozi wengi kushiriki na mambo yote yatakayojadiliwa ni muhimu kwa maendeleo na ufanisi kwa mahakama na kada ya sheria katika nchi.

Alisema ushiriki wa majaji na wataalamu utakuwa na mchango mkubwa wa kuwazidishia maarifa, uzoefu na kutanua wigo wa ushirikiano na wenzao katika nchi mbalimbali za Afrika.

Alisema serikali anayoiongoza itayatekeleza maazimio yanayohitaji kutekelezwa kwa upande wa Zanzibar na itashirikiana na mahakama za kikanda kwa yale mambo ambayo yanapaswa kutekelezwa kwa pamoja.

Pia, utekelezaji wa haki za binadamu umepewa kipaumbele na Serikali ya Zanzibar na Tanzania kama ilivyoelezwa katika Katiba ya nchi hizo.

"Tumeunda Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ambayo inaendelea kufanya kazi vizuri katika kuimarisha haki za binadamu katika pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tutaendelea kuhakikisha kwamba tunashirikiana ipasavyo na mahakama na jumuiya mbalimbali za kikanda na kimataifa zinazoshughulikia masuala ya haki za binadamu barani Afrika na duniani kote," alisema.

Naye Rais wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu, Imani Daud Aboud, alisema majadiliano katika ngazi za majaji mahakama za kikanda na kimataifa katika Afrika ni muhimu kwa ajili ya kubadilisha uzoefu wa kazi kutokana na kuwapo kwa mabadiliko mengi yanayoikabili dunia hivi sasa.

Aboud alisema maendeleo ya jamii hayawezi kupatikana bila ya kuwapo kwa misingi imara ya haki za binadamu na utawala bora ambayo yanatakiwa kutekelezwa na viongozi wa nchi za kiafrika. Rais wa Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki, Nestor Kayobera, aliwapongeza viongozi wa nchi za Afrika ya Mashariki wanaounda jumuiya hiyo kwa mchango wao mkubwa na kuiwezesha taasisi hiyo kufanya shughuli zake kwa ufanisi.

"Tunawapongeza viongozi wanachama wa nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kwa kutuunga mkono katika utendaji wa shughuli zetu za kusimamia haki na sheria katika chombo cha Mahakama ili kwenda na usawa wa binadamu," alisema.

## Watanzania wapoteza mabilioni mikopo ya wajasiriamali

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

MBUNGE wa Viti Maalum, Halima Mdee, amesema kwa miaka mitano kuanzia mwaka 2016/17 hadi sasa Watanzania wamepoteza Sh. bilioni 104 za mikopo ya wanawake, vijana na wenye ulemavu ambao hawajarejesha.

Akichangia mjadala wa Muswada wa Sheria ya Fedha mwaka 2022 jana, alisema ni muhimu serikali ikaweka wataalamu wa mikopo kutoa elimu, kufanya tathmini ya fedha zilizotolewa na kuja na mkakati mahsusi wa kuhakikisha hasara haipatikani tena.

Alisema ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), ya mwaka 2020/21, ilionyesha wanufaika wa vikundi katika mamlaka 155 za serikali za mitaa, hawakurejesha Sh. bilioni. 47.01.

Mdee alisema kuna halmashauri 185, kati ya hizo 155 fedha zilitolewa, lakini kuna shida kubwa ya marejesho.

Wakati akichangia Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Mwanaisha Ulenge, aliomba mwongozo na kumpa taarifa Mdee kuwa kuna mwongozo una upungufu wanalazimisha wakopaji kurejesha mkopo ndani ya mwaka mmoja, huku akitolea mfano aliyekopa Sh. milioni 10 anatakiwa kurejesha ndani ya muda huo jambo alilosema sio sahihi.

Mdee alisema tathmini ya miaka mitano kwa mujibu wa CAG, mwaka 2016/17, halmashauri 84 zilishindwa kurudisha Sh. bilioni 5.8, mwaka 2017/18, halmashauri 90 Sh. bilioni 10, mwaka 2018/19 halmashauri 110, Sh. bilioni 13.7, mwaka 2019/20, halmashauri 130, Sh. bilioni 27, mwaka 2020/21, halmashauri 155, Sh. bilioni 47 na kufanya jumla ya Sh. bilioni 104.

Alisema serikali ina wajibu wa kusimamia fedha hizo zitumike ili wapewe wanaostahili na wafanye marejesho stahiki wengine wapate.

Alisema mfuko wa vijana na wanawake ulikuwa wa kwanza kuanzishwa mwaka 1993, baadaye mwaka 2019 yakafanyiwa marekebisho ili kufanya mgawanyo wa sasa.

"Huu mfuko kwa ujumla wake una umri wa miaka 29, kama tuna mfuko wenye umri wa mtu mzima lazima tujiulize una matokeo gani katika kuondoa umaskini, na kutengeneza ajira za mtu mmoja mmoja ni jukumu la serikali kufanya tathmini ya kina kujua tumekosea wapi, tumepatia wapi na tutaboresha wapi.

Katika mapendekezo ya Bajeti ya mwaka 2022/23, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema serikali inadhamiria kupunguza asilimia hiyo ibaki tano ili igawanywe kwa mbili wanawake, vijana na moja kwa wenye ulemavu.

# Bibi auawa kwa kupigwa na kitu kizito kichwani

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

ELIZABETH Kibata (70) , mkazi wa Kitongoji cha Isanagongo, Kijiji cha Nyamigege, Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama mkoani Shinyanga, ameuawa kwa kupigwa na kitu kizito kichwani na kupoteza maisha papo hapo.

Imedaiwa na ndugu zake kuwa, bibi huyo alivamiwa na watu watatu usiku na mpaka sasa watuhumiwa hao hawajajulikana majina yao na hawajakamatwa.

Mtoto wa marehemu, Lucas Juma (50), akizungumza na Nipashe kwenye kitongoji hicho jana, alisema tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa sita usiku. Alisema kuwa kabla ya uvamizi huo, watu watatu walikwenda kwa marehemu majira ya asubuhi kwa madai ya kutafuta mashamba ya kununua katika familia hiyo.

Juma alisema kuwa baada ya kuvamia walianza kuingia chumba chake na kumwamuru ajifunike shuka na kumtoa mke wake nje na kumnyang'anya simu huku wakimhoji na kisha kumtaka arudi chumbani.

Alisimuliwa kuwa baadaye, watu hao waliingia chumba alichokuwa amelala bibi huyo na wajukuu wawili na kwamba alisikia sauti ya bibi huyo ikimwita lakini aliogopa kuitika. "Kabla ya kufanyika mauaji hayo, walifika watu watatu majira ya asubuhi, hawakumkuta mama yangu, alikuwa ametoka. Walimkuta mke wangu ambaye aliwapa majibu hayo na kumwomba namba za simu ili wampigie wajue alipokwenda.

"Baada ya kumkosa waliahidi watarudi tena majira ya saa nane mchana, lakini hawakutokea na usiku ndipo walipovamiwa na kumpiga na kitu kizito kichwani," Juma alisimulia.

Alidai kuwa baada ya kuona kumekuwa kimya, alinyanyuka na kwenda nje kisha kuingia chumba cha mama yake na kukuta sehemu ya kichwa imepondeka ndipo alipopiga kelele na kupiga simu kwa kiongozi wa kitongoji na ndugu wengine kuomba msaada.

Mwenyekiti wa Kitongoji hicho, Sumuni Elias, alisema alipigiwa simu majira ya saa saba usiku na mtoto wa marehemu kuwa wamevamiwa.

Hata hivyo, kiongozi huyo alisema kuwa katika kumdadisi mtoto huyo, alidai kulikuwa na mgogoro wa ardhi katika ukoo upande wa mama yake na watoto wa mjomba wake na kesi ilimalizwa katika baraza la ardhi na kutolewa hukumu.

Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Anthony Guta, alisema kuwa baada ya kupata taarifa juu ya tukio hilo la mauaji ya kikatili, alitoa amri ya wenyeviti wote wa vitongoji vinne na kamati ya ulinzi na usalama ya kijiji kuanza kufanya uchunguzi wa tukio hilo na kuwataka wananchi kutoa taarifa kwa viongozi wanapoona watu ambao hawawafahamu.

Mwenyekiti wa Waganga wa Tiba za Asili, Kata ya Busangi, Nkwabi Manyesura ( 70), alisema hilo ni tukio la tatu la mauaji ya aina hiyo katika kijiji hicho mwaka huu.

Aliomba serikali kudhibiti matukio ya ukatili kwa kuwa hivi sasa kila akisikiliza vyombo vya habari, anasikia watu wameuawa.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, George Kyando, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo, akifafanua kuwa chanzo cha uvamizi na mauaji hayo ni mgogoro wa ardhi katika familia.



Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, akitembelea makumbusho ya Gitega nchini Burundi juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CHADEMA yataka zuio mikutano ya siasa lifutwe

**Na Renatus Masuguliko,** GEITA

MKUTANO wa Kanda ya Ziwa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) uliofanyika mkoani Geita, umemalizika kwa kuiomba serikali kuondoa zuio la kutofanyika kwa mikutano ya hadhara ya kisiasa ili kutoa fursa ya kujiandaa kushiriki Uchaguzi Mkuu ujao.

Kanda hiyo ya CHADEMA inaundwa na mikoa mitatu ya Mwanza, Geita na Kagera.

Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, aliwasilisha hoja yao hiyo juzi wakati akifunga mkutano na kutoa majumuisho ya mkutano huo.

Mnyika alisema hali ya kisiasa kwa sasa ni nzuri lakini CHADEMA ingependa kuona zuio lililowekwa la kufanyika kwa mikutano ya hadhara ya kisiasa linaondolewa ili kuweka mazingira rafiki kwa ajili ya kutoa elimu kwa umma na kuwajengea uwezo wananchi kupiga kura.

Alisema CHADEMA inaridhia kuendelea kwa mazungumzo yanayoendelea kati ya Serikali ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na chama chao kwa lengo la kuleta maridhiano ya kisiasa nchini.

Alisisitiza kuwa suala la kupatikana kwa Katiba Mpya na Tume huru ya Uchaguzi ni ajenda endelevu kwa chama chao.

Awali, Mwenyekiti wa Baraza la Vijana wa CHADEMA (BAVICHA), John Pambalu, akimkaribisha Mnyika, katika mkutano huo, aliwashukuru wanachama wenzake na viongozi wa kada zote kwa kumuunga mkono katika operesheni yake ya kusaka Katiba Mpya, jukumu lililokuwa limekabidhiwa kwa BAVICHA na uongozi wa juu wa chama chao.

Mwenyekiti wa CHADEMA Mkoa wa Geita, Fabian Mahenge, aliyekuwa mwenyeji wa mkutano huo, alisema sasa kuna nuru iliyoanza kujitokeza ya matumaini ya hali ya kisiasa nchini, hasa kwa kambi ya upinzani na kuwa ni wakati mwafaka kwa upinzani kujijenga upya kwa ajili ya uchaguzi mkuu ujao.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## AZAKI zitimize wajibu wake fedha za Mfuko wa Jimbo

**MFUKO** wa Maendeleo ya Jimbo la Uchaguzi (CDCF) ulianzishwa kwa Sheria ya Mfuko huo ya Mwaka 2009 kwa lengo la kuchochea maendeleo ya jimbo.

Sheria hiyo inahusu majimbo yote ya uchaguzi Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar, usimamizi na uangalizi wake ukiwa chini ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais anayesimamia Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar, uko chini ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia Masuala ya Muungano, akisaidiwa na maofisa waangalizi wa fedha zitakapokuwa zimetumwa kwenye majimbo ya uchaguzi ya Tanzania Zanzibar.

Kulingana na matakwa ya kifungu cha 4(3) cha sheria ya mfuko huo, matumizi yote ya fedha kutoka kwenye mfuko yatapaswa kufanywa kulingana na matakwa ya Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001, Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2013 na Sheria ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo pamoja na kanuni zake.

Kifungu cha tano (5) cha Sheria ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo la Uchaguzi kinaelezea utaratibu utakaotumika katika kutenga fedha kwa ajili ya mfuko huu, pia taratibu za kufuatwa katika matumizi ya fedha hizo.

Huku kukiwapo taratibu za kuzingatiwa katika matumizi ya fedha, tayari kuna taarifa za matumizi mabaya ya fedha za mfuko huo katika baadhi ya maeneo nchini.

Mathalani, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) katika ripoti yake ya mwaka 2019/20, alibainisha kuwapo shida kwenye matumizi ya fedha za mfuko wa jimbo, baadhi zikitumika kutekeleza miradi ya vyama vya siasa na hata ya taasisi za dini isiyogusa wananchi moja kwa moja.

Hali hiyo sio tu kwamba ni matumizi mabaya ya fedha za umma, bali ni ishara ya kutokuwapo uwajibikaji miongoni mwa wanaopaswa kuusimamia Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo.

Sehemu ya tatu ya Sheria ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo inaelezea uwapo wa kamati ya kusimamia fedha za mfuko, itakayokuwa na wajumbe wasiozidi saba wakiongozwa na mbunge aliyechaguliwa na wapigakura wa jimbo husika la uchaguzi.

Nipashe pia tunatambua kwamba vipo vifungu ndani ya sheria hiyo vinavyoainisha wajumbe wengine wa kamati hiyo, wakiwamo maofisa watendaji kata kwa Tanzania Bara na masheha kwa Tanzania Zanzibar.

Tunakumbusha kwamba sheria hiyo inaelekeza mjumbe mmoja atakayeteuliwa na Kamati ya Mfuko wa Jimbo kutoka kwa Asasi ya Kiraia (AZAKI) iliyo hai na inayoendesha shughuli zake kwenye jimbo husika la uchaguzi, pia utaratibu wa kumpata ambao hufanywa wakati wa kikao chake cha pili baada ya kamati kuzinduliwa na kuanza rasmi shughuli zake.

Kwa kuzingatia matakwa haya ya kisheria, Nipashe tunazikumbusha AZAKI kuhakikisha zinatekeleza wajibu huu kwenye usimamizi na uangalizi wa mfuko huu, ili kuongeza uwajibikaji na ulinzi wa fedha za umma.

Tunaamini AZAKI zikiwajibika vizuri katika hili, ni wazi maslahi ya wananchi wa jimbo la uchaguzi yatazingatiwa kwa kuhakikisha kunakuwapo na usimamizi bora na uwajibikaji stahiki katika matumizi ya fedha za Mfuko wa Jimbo, ili kuwaletea wananchi maendeleo wanayostahili.

Mjumbe wa AZAKI katika kamati husika ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, anabeba wajibu mkubwa wa kuhakikisha fedha za mfuko zinatumika vizuri na kunakuwapo na thamani ya fedha kwa matumizi yote ya fedha za mfuko.

Nipashe tunaamini kwamba, kwa kufanya hivyo tu, kutakuwapo na maana ya uwapo wa mjumbe mwakilishi wa AZAKI katika jimbo la uchaguzi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Wizi huu unahitajika mbadala ulinzi shirikishi

Na Mwandishi Wetu

**WIZI** majumbani, kupora watu njiani, utapeli unaofanywa usiku na mchana kutumia simu na kwa ujumla kukosekana usalama ni masuala yanayolalamikiwa na wakazi wengi jijini Dar es Salaam.

Mathalani, zipo habari za vikundi vya wahalifu wanaojiita 'panya road' hawa wanadaiwa kuibuka na kupora popote na kuwaachia wananchi kilio.

Wapo majambazi wa simu wasio na majina wanaowatumia watu ujumbe wa kutaka pesa kila siku licha ya maelezo ya serikali kuwa namba zimesajiliwa tena kwa kielektroniki.

Wapo wanaofanikiwa kuwaibia mamia ya Watanzania ambao elimu ya utapeli wa simu haijawafikia.

Majambazi wanaoiba kwa kutumia silaha nao wamechachamaa, wanatishia maisha na biashara na wiki iliyopita polisi iliripoti kuua watatu wanaodaiwa walikuwa wanaelekea kuvunja duka la supermarket na kuiba huko Goba Tegeta A jijini Dar es Salaam.

Habari za wizi zinaibuliwa kila kona lakini mojawapo ya taarifa zilizoripotiwa karibuni ni madai ya kuwapo wizi unaofanywa eneo la Mbezi Msumi ambalo sasa ni kama kila nyumba imepitiwa na mali kuibwa.

Msumi ni eneo lililo karibu na Madale, likipakana na Tegeta A na Makabe. Wakazi wengi wa eneo hilo wanalalamikia kuibiwa kwa mfululizo televisheni za kileo maarufu 'flat screens', wanaibiwa mapazia na fimbo zake, pamoja funguo za nyumba zao na wezi hao wanaodaiwa kuwa hawana hofu.

Yako madai kuwa familia kadhaa ndani ya muda mfupi mwezi huu wa Juni zimeibiwa kwa utaratibu huo wa wezi kuchukua pazia nyumba nzima, fimbo za pazia hizo, simu, chaja, kuiba vifaa vya ujenzi kama marumaru (tiles), nguo za watoto na mabegi ya shule, kukiwa na hofu kuwa wanatumia dawa za usingizi.

Wapo ambao wameibiwa mpaka vyakula ndani ya friji na walipoamka alfajiri wamekuta milango iko wazi na mbwa wanakula vyakula ndani ya hotpot, vilivyokuwa vimetunzwa frijini.

Wizi huo unadaiwa kufanyika kupitia madirishani kwa kukata mabamba (flat bars) yanayotumiwa kutengeneza madirisha. Mabamba hayo yametumiwa na wengi badala ya nondo yanadaiwa ni mepesi na ni rahisi kukunjwa na kukatwa kwa kutumia 'plaiz' au vyuma vingine pamoja na vipande vya nondo.

Ukweli ni kwamba pamoja na kukata madirisha kuna madai kuwa hata funguo bandia zinatumiwa na pia kuna kemikali zinazopakwa kwenye vioo kuvilainisha na kurahisisha kazi ya kuingia ndani kupitia dirishani.

> **Aidha, ubunifu unaweza kuelekezwa kwenye kupiga picha na kuzituma kwenye simu za mwenye nyumba, majirani na polisi.**

Yanapoelezwa masuala ya wizi mara moja jibu ni ulinzi shirikishi, lakini pia nalo linakwamishwa na hali ya uchumi. Wananchi wa kawaida wanatakiwa kuchangia si chini ya Shilingi 3,000 kila mwezi kwa ajili ya walinzi.

Wenye magari nao huchangia Shilingi kuanzia 5,000 kwa walinzi hao. Ukweli ni kwamba ulinzi shirikishi unakwama, tatizo ni kipato kwenye familia nyingi, hazina fedha.

Hivyo, ni wakati wa kufikiria na kubuni mbinu za kisayansi na kiteknolojia kudhibiti wizi majumbani. Kama kuna taa zinazowakwa kwa 'sensa', mageti yanayofunguka kwa teknolojia hiyo, milango inayohisi adui ni vyema serikali, wadau wa utafiti, wabunifu, wafanyabiashara na polisi wanaojua mbinu za kitaalamu za kudhibiti wizi wakaleta teknolojia mbadala ya walinzi shirikishi.

Utaalamu unaweza kuhusisha mambo mengi ikiwa ni pamoja na taa za nyumba nzima kuzimika pale au kupiga kelele kifaa kinapohisi kuna uharibifu mfano kukatakata madirisha na kushika milango na vitasa au televisheni, ikibidi teknolojia ya alama za vidole nayo itumike.

Aidha, ubunifu unaweza kuelekezwa kwenye kupiga picha na kuzituma kwenye simu za mwenye nyumba, majirani na polisi.

Ni wakati wa kufikiria njia mbadala wa ulinzi shirikishi kupunguza ukubwa na kuzidi kuenea kwa tatizo.

## Wauzaji wa gongo, bangi watajwa kero Singida

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WATENGENEZAJI wa pombe kali ya kienyeji aina ya gongo na wauzaji bangi katika Kitongoji cha Njuki, Kijiji cha Mwagwanjuki, Kata ya Mandewa, Manispaa ya Singida, wametajwa kuwa kero kwa wananchi.

Kundi hilo limelalamikiwa na wananchi kwamba, wateja wao wakilewa, wanarusha ovyo mawe kwenye paa za nyumba za wakazi wa eneo hilo.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Binilth Mahenge, alipewa malalamiko hayo na mmoja wakazi wa kitongoji hicho wakati wa mkutano wa hadhara uliofanyika kwenye viwanja vya stendi ya zamani ya mabasi mjini hapa.

"Kero yangu Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa ni kuhusu wafanyabiashara wanaopika gongo na wauza bangi, usiku kucha wamekuwa kero. Mimi ni mzee mjane, huwa sipati usingizi kwa sababu utakuta wanarusha mawe juu ya nyumba mfululizo," alilalamika Mwajuma Rashid (80), mkazi wa kitongoji hicho.

Mwajuma alisema cha kushangaza kero wameshaiwasilisha kwa Jeshi la Polisi lakini watuhumiwa wakishakamatwa, wanaachiwa huru na kurejea mitaa kuendelea kazi zao kama kawaida.

Aliwasilisha kero nyingine ni kutopata msaada ikiwamo kuingizwa kwenye orodha ya wanufaika wa Mfuko wa Maendeleo Jamii (TASAF) kwa kuwa ni mjane na ana wajukuu anaowalea na hawana wazazi. Kufuatia malalamiko ya kero ya wauzaji gongo na bangi, Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Mahenge, alimwagiza Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Lucas Mwakatundu, kuhakikisha wanalifanyia kazi haraka suala hilo.

Kamanda Mwakatundu alimwahidi mkuu wa mkoa kuwa suala hilo litafanyiwa kazi kwa watuhumiwa wote kukamatwa na kuendelea kufanya doria eneo hilo.

# RC akunjua makucha waliotajwa na CAG

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, amemwagiza Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko na kamati yake ya ulinzi na usalama kuwasaka watumishi wote na watu wengine ambao wamekimbia baada ya kufanya ubadhirifu kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo.

Ubadhirifu huo ni ulioibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) katika ripoti yake kwa mwaka 2020/21 uliowasilishwa bungeni Aprili 12, mwaka huu.

Sophia alitoa maagizo hayo juzi kwenye kikao maalum cha Baraza la Madiwani Manispaa ya Shinyanga kilichojadili taarifa ya CAG na kusomwa taarifa kuwa baadhi ya hoja zilizoshindwa kujibiwa kwa sababu watu waliofanya ubadhirifu wa fedha kwenye miradi, wamekimbia na hawajulikani waliko.

Alimwagiza mkuu wa wilaya na kamati yake kuhakikisha watu wote ambao wametajwa kufanya ubadhirifu huo na kukimbia, wanasakwa.

Alisema lazima watu hao wapatikane na kurudisha fedha walizotafuna.

"Mkuu wa wilaya kaa na kamati yako na ulinzi na usalama mhakikishe watu wote hawa ambao wamekimbia baada ya kufanya ubadhirifu na kusababisha hoja za CAG wapatikane, mkishindwa tuleteeni sisi kwenye kamati yetu ya ulinzi na usalama mkoa tuwasaidie kufanya hivyo," aliagiza.

Katika hatua nyingine, Sophia amewataka watendaji wa halmashauri wawe wanajibu hoja za CAG.

"Tunataka halmashauri zetu ziendelee kupata hati safi, lakini hoja ziwe chache na kufutika kwa sababu mkoa wetu wa Shinyanga ni kati ya mikoa 10 nchini ambayo ina hoja nyingi za ukaguzi wa CAG," alisema.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Shinyanga, Zuwena Omary, alisema Mkoa wa Shinyanga ni wa tatu kati ya 10 kuwa na hoja nyingi za CAG, na kubainisha kuwa tayari wameshajipanga ili kuhakikisha zinapungua, huku akiwataka watumishi waongeze juhudi katika uwajibikaji.

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, aliwataka watumishi wa serikali wawe waadilifu katika utekelezaji wa majukumu yao, kutunza nyaraka za miradi wakati wa ununuzi pamoja na kupeleka benki fedha za makusanyo ya mapato ili kupunguza wingi wa hoja kutoka kwa CAG.

Awali Mwekahazina wa Manispaa ya Shinyanga, Nicksoni Itogoro, akisoma taarifa ya CAG kwenye baraza madiwani, alisema ubadhirifu wa fedha katika ujenzi wa ofisi ya Kata ya Kambarage Sh. milioni 13 na mhusika alishakimbia na hajulikani alipo.

Alitaja hoja nyingine ni matumizi yasiyokuwa na tija, kwamba halmashauri ilitumia Sh. milioni 19.2 kununua eneo la ujenzi wa bwawa la maji taka katika machinjio ya kisasa Ndembezi, lakini halifanyi kazi iliyokusudiwa.

Hoja nyingine ni upungufu kwenye mikataba ya ukusanyaji ushuru na kutopelekwa fedha za makato ya mishahara ya wafanyakazi wa serikali kwenye Mfuko wa PSSSF Sh. milioni 5.9. Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga, Jomaary Satura, alisema katika majibu ya ukaguzi yaliyotolewa na CAG kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 30 mwaka jana, manispaa hiyo ilikuwa na hoja 79 na imejibu 38 na kuzifuta, huku 41 zikiwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Baadhi ya Madiwani wa Manispaa ya Shinyanga walisema hoja ambazo zimekuwa zikijirudia mara kwa mara, zifanyiwe kazi na kufutwa pamoja na kusakwa kwa watumishi ambao wamefanya ubadhirifu wa fedha na kukimbia na kusababisha kuibuliwa kwa hoja kwenye miradi.


**JADA INVESTMENT LIMITED NA STEAM GENERATION RECOVERIES LTD**

## NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya **JADA INVESTMENT LIMITED na STEAM GENERATION RECOVERIES LTD** Kwa Idhini tuliyopewa na **MWANGA HAKIKA MICROFINANCE BANK LIMITED** tunatoa muda wa siku 14 wadaiwa waliorodheshwa kwenye jedwali hapo chini wawe wamelipa madeni wanayodaiwa na **MWANGAHAKIKA MICROFINANCE BANK LIMITED,** Kinyume na hapo tutalazimika kuuza kwa njia ya mnada wa hadhara mali walizoweka kama dhamana ya mkopo. Mnada utafanyika Mahali dhamana ilipo kama ifuatavyo.

| S/NO | JINA LA MDAIWA | AINA YA DHAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA | TAREHE /MUDA |
|---|---|---|---|---|
| 01 | Rose Emmanuel Gadau | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Mloganzila Kwembe-Manispaa ya Ubungo | 30/07/2022; 10:00 asubuhi |
| 02 | Edward John Nkalu | Nyumba yenye hati | Kisukulu B-Segerea, Manispaa ya Ilala. | 16/07/2022; 10:00 asubuhi |
| 03 | Yohana M Maridadi | Nyumba yenye leseni ya makazi | Yombo Vituka-Manispaa ya Temeke | 23/07/2022; 10:00 asubuhi |
| 04 | Mwema khamis Mwamvura | Gari lenye nambari ya usajiri T 696 CFP | Mbezi Beach | 12/07/2022; 12:00 mchana |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe ya Tangazo hili
2. Dhamana itauzwa kama ilivyo
3. Mnunuzi atakayeshinda anapaswa kulipa 25% ya bei aliyofikiwa siku ya mnada, na 75% aliyosalia atalipa ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada, kinyume na hapo kiasi kilichotolewa awali hakitarudishwa na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha hati miliki (transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa ni la mnunuzi.
5. Mnada utafanyika mahali ambapo dhamana zilipo na si vinginevyo.

**KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA NAMBA**

| | | |
|---|---|---|
| Mkurugenzi Mtendaji | Mkurugenzi Mtendaji | Mwanga Hakika Bank |
| Jada Investment Limited | Steam Generation Recoveries ltd | S.L.P 11735 |
| S.L.P 69098 | S.L.P 80607 | Dar es Salaam |
| Dar es Salaam. | Dar es Salaam. | Namba za Simu |
| Namba za Simu; 0788493699/ 0679527995 | Namba za Simu; 0715917451 | 0678019509 |

216921401



**IN THE HIGH COURT OF UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MOSHI DISTRICT REGISTRY**
**AT MOSHI**
**PETITION NO. 4 OF 2021**
**IN THE MATTER OF THE COMPANIES ACT NO. 12 OF 2002**
**AND**
**IN THE MATTER OF MSOKE NASHALO FARMS LIMITED**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE PETITION FOR WINDING UP BY COURT OF "A COMPANY" MSOKE NASHALO FARMS LIMITED**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE PETITIONER WHO IS A CONTRIBUTORY OF MSOKE NASHARO FARMS LIMITED**
**DAPHROSA EDITH MUSHI..............PETITIONER**
**VERSUS**
**MSOKE NASHALO FARMS LIMITED.................RESPONDENT**

**DRAWN ORDER**

**WHEREAS:-** The petitioner has filed the petition under section 275,279 (1), (b)(d)(e) and 281 of the Companies Act Cap 12 [R.E 2002] and Rule 90 (1) and (2) of the Companies (Insolvency) Rules, 2005 moving the court for the following orders:-

(i) That, Msoke Nashalo Farms Limited be wound up by the Court under the provisions of the Companies Act, No.12 of 2002.
(ii) That, Hellen Mahuna & Jeremiah Tarimo, be appointed liquidators to take over the the control of the assets and liabilities of the Company.
(iii) Cost for the Petition be provided for.
(iv) Further, orders to be made and given by this Court as it deems fit and just to grant.

**AND WHEREFORE: -** The Application is coming for Ruling before Hon.B.R. Mutungi, J. this 2nd day of June, 2022 in presence of Mr. Charles Mwangani holding brief for Mr. Jeremiah Tarimo for the respondent and in absence of the petitioner dully notified.

**THIS COURT DOTH HEREBY ORDER THAT:-**

1. MSOKE NASHALO FARMS LIMITED, a Limited Liability Company, incorporated in Tanzania on 23/04/1983 through a Certificate of Incorporation No.9337 with its registered office at House No.44, Chagga Street Moshi Tanzania is to be wound up under the provisions of section 279 (1) of the Companies Act.
2. Ms. Hellen Mahuna and Jeremiah Tarimo are hereby appointed as liquidators to take over control of the assets and liabilities of the Company in terms of Section 294 of the Companies Act Cap. 12 R.E. 2002.
3. No order for costs.

Given under may Hand and Seal of the Court this 2nd day of June 2022.

June, 2022.

**B.R. MUTUNGI**
**JUDGE**
**2/06/2022**
**Issued on 13TH day of June, 2022**

216921201

# COSTECH yatangaza fursa ya bilioni 20/- kwa watafiti

**Na Mwandishi Wetu**

WATAFITI kutoka nchi 11, ikiwamo Tanzania, watachuana kuzipata Euro milioni nane (Sh. bilioni 19.623) zilizotengwa na Baraza la Kimataifa la Utafiti (GRC) kufadhili miradi itakayoshinda kwa lengo la kuchochea utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG).

Fungu hilo pia limetengwa ili kuchochea utekelezaji wa malengo hayo katika maeneo sita ya maendeleo ya jamii; ustawi wa uchumi; chakula na lishe; upatikanaji wa nishati duniani; maendeleo ya miji; na masuala ya mazingira.

Akizungumza na waandishi wa habari mkoani Dar es Salaam jana kuhusu mradi huo, Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia, Dk. Amos Nungu, GRC imejizatiti kuhakikisha inashiriki kuchochea utekelezaji wa SDG kupitia ubunifu na utafiti.

Alisema kuwa kupitia mradi huo, watafiti kutoka Tanzania wataungana na watafiti wenzao kutoka mataifa mengine 10, hivyo kuwa na fursa adimu ya kubadilishana uzoefu wa kimataifa katika kukabiliana na vikwazo mbalimbali.

Dk. Nungu alisema watafiti watapaswa kuungana kwa kuwa na timu zinazojumuisha walau nchi tatu kwa lengo la kufanya utafiti wa pamoja ili utafiti uwe bora na wenye matokeo chanya.

"Ufatiti na matokeo yake lazima yailenge jamii na kuinua maisha ya watu katika maeneo tajwa," Dk. Nungu alisema. Alizitaja nchi ambazo watafiti wake watachuana kupata ufadhili huo ni Chile, China, Côte d'Ivoire, Kenya, Norway, Afrika Kusini, Uswisi, Sweden, Tanzania, Uholanzi na Uturuki.

Alisema maelekezo kwa watafiti wanaotaka kushindana kupata ufadhili huo, yanapatikana katika tovuti rasmi ya COSTECH na kwamba mifumo ambayo nchi washirika zimekubaliana kuitumia wakati wa utekelezaji wa mradi huo ni ya Afrika Kusini.

Dk. Nungu alisema COSTECH itawawezesha washiriki kutoka Tanzania kupata mawasiliano na washiriki wengine kutoka mataifa tajwa ya mabara manne, pia kuwaongezea ujuzi ili kuboresha zaidi mawazo yao.



Mabalozi wa kodi wa hiari wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Subira Mgalu pamoja na Zulfa Mmaka wakitembelea ujenzi wa majengo ya Chuo cha Ufundi kinachojengwa jijini Dodoma katika ziara ya kikazi kuonyesha namna matumizi ya kodi za wananchi zinavyofanya kazi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mabalozi wa kodi watembelea miradi nchini

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MABALOZI wa kodi wamewashauri Watanzania kulipa kodi ili kuiwezesha serikali kutekeleza miradi ya maendeleo kupitia bajeti iliyopangwa ya Sh. trilioni 41.48 kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Wabunge mabalozi wa kodi walitoa rai hiyo jana wakati wa ziara yao mkoani Dodoma ya kutembelea baadhi ya miradi inayotekelezwa kwa kodi za wananchi.

Miradi iliyotembelewa na mabalozi hao ni pamoja na ujenzi Soko la Machinga, Mji wa Serikali 'Magufuli City', Chuo cha Ufundi cha Dodoma na ujenzi wa barabara za mzunguko.

Balozi wa Kodi na Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Pwani, Subira Mgalu, alisema kwamba katika kuchochea maendeleo ya nchi, ni vyema kuiunga mkono serikali kwa kulipa kodi kwa hiari.

"Kwa bajeti ya mwaka 2022/23, serikali imepanga kukusanya Sh. trilioni 41.48 ambazo zinakusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Mamlaka za Serikali za Mitaa, hivyo ili kufikia lengo la kukusanya fedha hizo, ni muhimu walipakodi na wananchi kwa ujumla wakalipa kodi kwa hiari na wakati," alisema Balozi Subira.

Alisema kuwa tangu Rais Samia Suluhu Hassan aingie madarakani, ameweka karibu sekta binafsi na kusisitiza kuwa serikali haifanyi biashara lakini imekuwa ikiandaa mazingira wezeshi ya ulipaji kodi kwa hiari.

Akizungumzia miradi aliyoitembelea balozi huyo, alisema thamani ya fedha imeonekana dhahiri na kusisitiza kuwa shughuli zitakazofanyika katika miradi hiyo zitakuwa na mwendelezo wa kuchangia Pato la Taifa na kuongeza mapato ya Halmashauri ya Jiji la Dodoma.

"Nitoe wito kwa wafanyabiashara wa kada mbalimbali wakubwa, wa kati na wadogo pamoja na Watanzania wote tuendelee kulipa kodi kwa hiari, tuendelee kudai risiti kila tunapofanya ununuzi na wafanyabiashara watoe risiti kila wanapouza bidhaa zao.

"Niwathibitishie Watanzania kwamba, endapo tutaendelea na uzalendo wa kulipa kodi kwa hiari ikiwa ni zile zinazokusanywa na TRA na kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa, nchi yetu itapiga hatua kubwa ya maendeleo", alieleza.

Balozi mwingine wa Kodi na Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Kusini Pemba, Zulfa Omary, alisema maendeleo ya nchi yoyote yanafikiwa kutokana na watu kulipa kodi.

"Ninawaomba Watanzania msiwaogope TRA wanapokuja kuhamasisha ulipaji kodi, kwa sababu manufaa ya kodi yameonekana katika miradi yote ambayo tumeitembelea katika ziara yetu, hivyo nawashauri na kuwasihi wananchi kuendelea kulipa kodi kwa hiari kwa sababu matokeo ya kodi mnazolipa yanaonekana waziwazi," alisema Balozi Zulfa.

Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipakodi wa TRA, Richard Kayombo, alisema ziara hiyo ililenga kuonyesha namna kodi zinazolipwa na wananchi zinavyotumika katika kuleta maendeleo.

"Mara nyingi tumekuwa tukiwahamasisha wananchi kulipa kodi, lakini safari hii imebidi tuwapitishe mabalozi wa kodi kwenye miradi mbalimbali inayotekelezwa na kodi hizo ili Watanzania nao waone kupitia vyombo vya habari jinsi kodi zao zinavyofanya kazi," alifafanua Kayombo.

## Kampeni 'Chora Ramani' kukomesha ukatili kijinsia

**Na Sabato Kasika**

KITUO cha Sauti ya Jamii Kipunguni, jijini Dar es Salaam kinachopambana na ukatili ndani ya jamii, kimetambulisha kampeni ya kujengea uwezo wanajamii, katika mambo mbalimbali ikiwamo kuzuia vitendo vya ukatili.

Mkurugenzi wa kituo hicho, Seleman Bishagazi, aliliambia gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, kuwa kampeni hiyo iliyopewa jina la 'Chora Ramani', itaendeshwa na vikundi vilivyoko kwenye jamii na mitandao ya kijamii.

Bishagazi alitaja vyombo vingine kuwa ni magazeti na televisheni, viongozi wa dini na wa vyama vya siasa na Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto (MTAKUWWA).

Alifafanua kuwa kampeni hiyo iliyoanza baada ya maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika, imeshafika kata za Mzinga, Majohe, Kimara, Kipunguni na Msongola.

Alisema lengo la 'Chora Ramani', ni kutaka kila mtu kwa nafasi yake kabla ya kufanya jambo lolote, anachora ramani itakayomsaidia kujua anachojiandaa kukifanya.

"Mtu anatakiwa kutafakari kwanza na kufanya uchambuzi kabla ya kutenda, hatua hii itamsaidia kuonyesha matokeo ya kile anachokusudia kukifanya," alisema Bishagazi.

Pia kampeni ya Chora Ramani, inatarajia kusaidia wazazi na walezi jinsi ya kuibua vipaji na ndoto za watoto wao kuchora ramani inayoonyesha njia za kuzifikia.

"Kampeni hii inalenga kusaidia jamii kuchora ramani itakayoonyesha faida za kila mtu kushiriki katika kuzuia vitendo vya ukatili na kujengea uwezo vikundi na watu binafsi njia ya kupita na kufikia malengo," alisema.

Kiongozi wa vijana Mtaa wa Nzasa Kimara, Asha Msango alisema, kampeni hiyo imekuja wakati muafaka hasa wakati huu ambao baadhi ya watu wanafanya uamuzi bila kutafakari kwanza.

"Ni imani yangu kwamba, watu wataizingatia, ili iweze kuleta matokeo chanya, hasa kwa upande wa vitendo vya ukatili katika jamii, ambavyo vimekuwa vikiongezeka kila kukicha," alisema Msango.

Sea Temba, kiongozi wa vikundi vya vikoba kutoka Kata ya Majohe, alisema kuna haja ya watu kuwa na hofu ya Mungu badala ya kuwaogopa binadamu.

Alisema, serikali imekuwa ikiandaa mikakati mbalimbali ikiwamo kuanzisha MTAKUWWA, ili kutokomeza vitendo vya ukatili, na kuwa kampeni hiyo inafaa kila eneo na itakuwa na mchango mkubwa.

**IN THE MATTAER OF MSOKE NASHALO FARMS LIMITED**
**AND**
**IN THE MATTAER OF THE COMPANIES ACT NO. 12 OF 2002**

**NOTICE TO CREDITORS**

**NOTICE** It is hereby given to the general public that by an Order of the court **(Hon. Mutungi, J)** dated 13th June, 2022, the high court of Tanzania (Moshi District Registry) in petition No. 4 of 2021 ordered that the affairs of **MSOKE NASHALO FARMS LIMITED** (the "company") be wound up by the court in accordance with the provisions of the companies Act, 2022

**FURTHER NOTICE** is given that

1. We, **Hellen Mahuna** of P.O.Box 1462 Moshi, Kilimanjaro, Tanzania and **Jerimiah Tarimo** of P.O.box 15159 Dar es Salaam, Tanzania were appointed liquidators by the court for purposes of winding up the company.
2. ALL creditors of the company, if any, are hereby asked to furnish to the liquidators with full details of their claims against the company at the address shown below within fourteen (14) days from the date of publication of this notice. The claim (if any) shall be presented in the form known as " proof of debt"(Form 365a) which is obtained at the office of the registrar of companies (Business Registrations and Licensing Agency-BRELA) or can be downloaded from the website of BRELA (www.brela.go.tz)
3. A meeting of all creditors of the company (if any) will be held at the address below on 28th July, 2022 at 10.00am

NSSF KILIMANJARO COMMERCIAL COMPLEX, 2ND FLOOR ROOM NO.5, MOSHI, KILIMANJARO TANZANIA.

**SIGNED at Moshi this 17th day of June, 2022**

……………………
Hellen Mahuna
For and on Behalf of Liquidators.

216921301

## Waomba elimu ya hedhi kwa wazazi

**Na Julieth Mkireri,** CHALINZE

MASHIRIKA yanayotoa elimu ya afya na hedhi salama ikiwa ni pamoja na matumizi ya taulo za kike, yameombwa kufikisha elimu hiyo kwa wanawake wa kabila la Kimasai ili watoto wao wa kike wazitumie taulo hizo na kuachana na utaratibu wa awali unaowanyima uhuru.

Jana katika Kijiji cha Switikona kilichoko Chamakweza, Halmashauri ya Chalinze wakati uzinduzi wa kampeni ya 'Hedhi Yangu Utu Wangu' inayoendeshwa na Youth Volunteer Network Development (YOVONED), baadhi ya mabinti kutoka kabila hilo, walipaza sauti kuhusu elimu hiyo, akisema inahitajika kwa kabila hilo ili kubadili mtazamo uliopo.

Mmoja wa mabinti hao, Roida Lowasa, alisema mila iliyojengeka katika kabila lao ukiwa kwenye hedhi ni jambo la aibu na wazazi wengine wakiona umeanza kupata hedhi, hata kama unasoma, wanakukatisha masomo na kukuozesha.

"Vikwazo ambavyo tunapitia sisi mabinti kwenye kabila letu kuongelea masuala ya hedhi ni kitu cha aibu sana na taulo za vitambaa hivyo hivyo.

"Sisi tunachoomba wa kuwapa elimu ya taulo za kike ni mama zetu kabla ya mabinti kwa sababu tukipewa sisi elimu kwenda kuwaelimisha, mama zetu wataona tunawavunjia heshima," alisema.

Blandina Bimu anayetoka kwenye jamii hiyo ya Kimasai, aliishukuru serikali kwa elimu ya afya ambayo wanaendelea kupatiwa kuhusiana na matumizi ya taulo za kike, akiomba isambae zaidi kwa jamii hiyo inayoishi vijijini ili kubadili mtazamo wao.

Blandina pia alisema kwa sasa wanawake wanapata matatizo ya matumbo na vizazi kutokana na maji ya mabwawa wanayotumia na hivyo kuiomba serikali kufanyia kazi suala la kuwafikishia maji safi kwenye eneo lao.

Mkurugenzi wa YOVONED, Philemon Mabuga, alisema taasisi hiyo baada ya kuzindua kampeni yao, wanalenga kuiendesha kwa miezi sita na kuwafikia mabinti 1,000.

Alisema mradi huo unatekelezwa na taasisi hiyo kwa kushirikiana na Women Connect Tanzania na wanatarajia kutoa elimu hiyo kwa kuhamasisha matumizi ya taulo za kike kwa afya zao.

Mabuga alisema kuwa wanaihamasisha jamii kuchangia ili kupata taulo nyingi za kike na kuwezesha kila binti kati ya walengwa 1,000 kupata pakti sita kwa ajili ya kipindi cha miezi sita.

Salma Muya kutoka kampuni ya Papertua, wazalishaji wa taulo za kike, alisema wameanza kutoa elimu hiyo kwa jamii ya Kimasai ili wazazi wabadilike na kuwaruhusu watoto wao wa kike kutumia taulo za kike badala ya vitambaa.

# TASAC kuboresha mazingira katika kazi za mabaharia

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

SHIRIKA la Wakala wa Meli Tanzania (TASAC) limepanga kuboresha mazingira ya kazi za mabaharia kwa kuona umuhimu wao wa kukuza uchumi wa nchi.

Hatua hiyo imetokana na kuwapo ongezeko la mabaharia wanaofanya usafirishaji wa mizigo ya wananchi kwenye bahari, ziwa na mito inayopatikana nchi.

Akizungumza mwishoni mwa wiki, Meneja Masoko Uhusiano na Umma kutoka TASAC, Josephine Bujiku, alisema, shirika limeendelea kuwa karibu na mabaharia kuzungumzia matatizo yaweze kufanyiwa kazi kwa maboresho ya maisha yao.

Bujiku alisema kwa kutambua sekta ya ubaharia ni muhimu, imeendelea kuzalisha wafanyakazi wenye kukuza uchumi wa nchi kupitia usafiri wa majini, kurahisisha na kupunguza gharama za ubebaji wa mizigo nchi kavu.

"Kwa Januari 2021 hadi Desemba vimetolewa vyeti 11,517 sawa na asilimia 181 ikilinganishwa na 2,098 kati ya Januari hadi Desemba 2020," alisema Bujiku. Baharia kutoka Bandari ya Dar es Saalam aliyefika kwenye maadhimisho ya mabaharia duniani ambayo kitaifa yalifanyika mkoani kagera, Amina Zakumera, alisema kupitia maadhimisho hayo, itasaidia wanawake kujitokeza zaidi kusomea sekta hiyo.

Alisema, hapo awali kazi ya ubaharia ilitambuliwa kuwa ni ya wanaume, lakini sasa kila mmoja ana uwezo wa kufanya shughuli yoyote ya kuzalisha uchumi.

"Niseme tu sasa hivi kazi ndiyo inatafuta mtu na hasa akijishughulisha katika kile alichokisomea na kujiunga kwenye vikundi mfano sisi wanawake mabaharia hapa nchini tuna chama chetu cha UMESA wanaofanya kazi baharini," alisema Zakumera.

Alisema, kazi hiyo inawafanya kujituma na kuamka kufanya sehemu ambazo walidhani kuwa wanaume ndiyo walistahili pekee.

Vile vile, alisema kwenye maeneo ya kazi hakuna sehemu isiyokuwa na matatizo au ugumu, lakini mwajiriwa atafuata sheria ambazo zipo na kuona wepesi wa kutimiza kile alichopangiwa kufanya na kupata.

Katibu Tawala wa Mkoa Kagera, Prof. Faustine Kamzora, aliyekuwa mgeni rasmi alisema, mabaharia ndiyo wenye nguzo kubwa ya kukuza uchumi, asilimia 90 ya usafirishaji duniani hubebwa na usafiri wa meli kwa gharama ndogo.

Alisema Tanzania ina mabaharia 5,300 kati yao ni asilimia moja pekee wa jinsi ya kike na kupendekeza ipo haja ya kutembelea shuleni kukutana na wanafunzi kuwapa elimu ya umuhimu wa mabaharia kwa jinsi zote.




Mkuu wa Idara ya Wateja Binafsi wa Benki ya NMB, Aikansia Muro (wapili kulia), akimkabidhi Mthamini Mkuu wa Serikali, Evelyne Mugasha (watatu kushoto), vipeperushi vyenye maelezo ya mikopo ya nyumba inayotolewa na NMB, alipofika kufungua warsha iliyoandaliwa na benki hiyo kwa wananchi wa Mkoa wa Dodoma jana. Wengine kutoka kushoto ni Meneja wa Mikopo ya ujenzi Benki ya NMB, Miranda Lutege, Meneja wa Kanda ya Kati, Nsolo Mlozi na Mkuu wa Idara ya Wateja Maalumu (kulia), Getrude Mallya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwalimu mstaafu alilia eneo la makaburi ya ndugu

**Na Thobias Mwanakatwe,** IKUNGI

MWALIMU Mkuu mstaafu wa Shule ya Msingi Wibia, kijiji cha Wibia Wilaya ya Ikungi mkoani Singida, Patrick Lissu, ameiomba serikali kuingilia kati na kumpatia eneo lake lililochukuliwa na shule ambalo lina makaburi 16 walipozikwa ndugu zake.

Alitoa ombi hilo kwa Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Jerry Muro, wakati wa mkutano wa viongozi wa halmashauri za vijiji, madiwani, wenyeviti na watendaji wa Kata ya Puma, wilayani humo katika ziara yake ya kusikiliza kero.

Lissu ambaye kwa sasa ni Mjumbe wa Serikali ya Kijiji cha Wibia, alisema amekuwa akifuatilia suala hilo kwa miaka minne tangu mwaka 2018 kwa viongozi wa kijiji, kata na ofisi ya Mkuu wa Wilaya bila mafanikio.

Alisema eneo hilo lenye makaburi lililochukuliwa tangu 1994 lina ukubwa wa ekari moja na lilichukuliwa wakati wa kuweka mipaka ya shule na kuzidishwa wakati wa kupima na kuchukuliwa eneo lenye makaburi ya familia.

"Eneo hili lililochukuliwa lina makaburi 16 walipozikwa ndugu zangu kuanzia 1948 akiwamo bibi, babu, baba na mama yangu mzazi, kaka zangu, hata kabla Shule ya Msingi Wibia haijaanzishwa," alisema.

Ombi la kutaka arejeshewe eneo hilo baada ya kushindikana kutoka serikali ya kijiji na kata, aliliwasilisha kwa aliyekuwa Mkuu wa wilaya hiyo, Miraji Mtaturu ambaye kwa sasa ni Mbunge wa Singida Mashariki.

Alisema Mtaturu alimwagiza Ofisa Tarafa afuatilie suala hilo ili apewe haki yake, lakini bahati mbaya hadi anaondoka kwenye ukuu wa wilaya halikushughulikiwa.

Aliongeza kuwa baadaye wilaya hiyo ilipopata Mkuu wa Wilaya mwingine, Edward Mpogolo, alimwandikia barua kuhusu suala hilo naye alimwagiza Ofisa Ardhi alishughulikie.

Hata hivyo, suala hilo halikupatiwa ufumbuzi kwa kuwa wakati Ofisa Ardhi anafuatilia suala hilo baadhi ya nyaraka hazikuonekana katika serikali ya kijiji, lakini yeye (Lissu) alitoa barua ambazo zilidhihirisha kuwa eneo hilo ni la familia na lina makaburi.

"Mheshimiwa DC (Jerry Muro) wewe utakuwa ni wa tatu sasa kuwasilisha lalamiko langu hili kwako, ombi langu nipewe eneo la makaburi ya ndugu zangu ambalo limechukuliwa na shule," alisema Lissu.

Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Muro baada ya kusikiliza maelezo hayo alimwagiza Ofisa Tawala wa Wilaya papo hapo kumwandikia barua haraka Lissu ili aweze kukabidhiwa eneo hilo la makaburi.

Kutokana na agizo la Mkuu wa Wilaya, Mwalimu Mkuu huyo mstaafu alimshukuru DC Muro kwa kuanza kufuatilia suala hilo.

# Treni ya mwendokasi kuanza rasmi Septemba

BUNGE limeelezwa kuwa treni ya mwendokasi kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro itaanza rasmi kufanya kazi Septemba, mwaka huu.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Atupele Mwakibete, alieleza hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Christine Ishengoma.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji lini treni ya mwendokasi kutoka Dar es salaam hadi Morogoro itaanza.

Atupele alisema reli ya SGR kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro ina urefu wa kilometa 300 na itaanza kufanya kazi rasmi Septemba, mwaka huu.

"Mwezi wa nane (Agosti mwaka huu) yataingia mabehewa na vile vichwa kwasababu sasa hivi kinachofanyika ni majaribio, kituo kwa kituo, stesheni kwa stesheni, umeme, signal (alama) ndio kinachofanyika kwa wakati huu," alisema.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Taska Mbogo, alihoji lini serikali itaanza ujenzi wa treni ya mwendokasi kutoka Kaliua-Mpanda hadi Karema.

Naibu Waziri alisema katika bajeti ya mwaka wa fedha 2022/23, serikali imetenga fedha kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) kipande cha Kaliua-Mpanda hadi Karema.

Mwakibete alisema serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania (TRC), imekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa njia ya reli ya Kaliua-Mpanda-Karema kwa kiwango cha Standard Gauge (SGR).

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Fatma Toufiq, alisema reli hiyo ni muhimu kwa ukanda wa Kusini Magharibi na ni muhimu kwa usafirishaji mizigo wa nchi jirani za Kongo, Burundi na Rwanda.

"Je, serikali haioni umuhimu sasa wa kuharakisha ujenzi wa reli hii ili wananchi wa maeneo hayo wapate tija," alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri alikiri serikali inatambua umuhimu wa reli hiyo na mizigo mingi inatoka kwenye hizo nchi.

Alisema kwa mwaka wa fedha ujao, serikali imetenga Sh. milioni 199.4 ili kuanza ujenzi huo.

Katika swali lingine la nyongeza, Mbunge wa Vwawa (CCM), Japhet Hasunga, alisema kuna treni ya Tazara inatoka Dar es Salaam hadi Tunduma na kuhoji mpango wa serikali wa kupanua reli hiyo ili kuwa ya mwendokasi na kukidhi mahitaji ya eneo la Nyanda za Juu Kusini.

Mwakibete akijibu swali hilo, alisema reli hiyo ni ya nchi mbili za Tanzania na Zambia na kumekuwapo na kero mbalimbali kwenye uendeshaji wa reli hiyo.

"Habari njema ni hii ndani ya mwezi huu ifikapo tarehe 30, mawaziri wa pande zote mbili kutoka Tanzania na Zambia watakutana na pili tunataka kubadili sheria kwa kuwa sheria inayotumika kwa sasa ni ile iliyotungwa tangu kuanzishwa kwa Tazara, sasa Tanzania ikitaka kuwekeza ile sheria inabana," alisema.

"Maandalizi ya mabadiliko ya sheria hii yameshapitishwa tunasubiri kikao cha mawaziri hao ili tuhuwishe hii reli."



Mbunge Halima Mdee akizungumza bungeni alipokuwa akichangia mjadala wa kupitisha muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2022, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Serikali yabanwa kukarabati majengo mahakama

WABUNGE wameibana serikali kuhusu kujenga na kukarabati majengo ya mahakama hususan ya Mwanzo kutokana na maeneo mengine kulazimika kutumia Ofisi za Watendaji Kata na Tarafa kutoa huduma kwa wananchi.

Wakiuliza maswali bungeni jana, Mbunge wa Viti Maalum, Esther Bulaya, alisema katika Wilaya ya Bunda Mahakama za Mwanzo zina hali mbaya na Nasmo Jimbo la Mwibara wanatumia Ofisi ya Kata na Mgeta Jimbo la Bunda Vijijini na Kabasa zote zina hali mbaya.

Naye Mbunge wa Kilwa Kaskazini (CCM), Fransis Ndulane, alisema katika Tarafa ya Kipatimo jimboni humo shughuli za mahakama za mwanzo zimekuwa zikiendeshwa kwenye ofisi ya ofisa tarafa.

Kadhalika, Mbunge wa Tabora Mjini (CCM), Emmanuel Mwakasaka, alisema Mahakama za Mwanzo kwenye jimbo hilo ni chakavu ikiwamo Isevya hali ambayo mvua ikinyesha mahakimu wanashindwa kuingia kutoa huduma kutokana na maji kujaa.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Geofrey Pinda, alikiri kuwa mahakama nyingi zimechakaa hasa za Mwanzo.

Alisema serikali inakwenda kuanza ujenzi wa mahakama ngazi ya makao makuu ya tarafa na mpango wa ukarabati unaendelea nchi nzima kwenye majengo yanayofaa kukarabatiwa. "Mahakama nyingi za mwanzo majengo yake yalijengwa miaka ya nyuma sana na yanahitaji ukarabati mkubwa sana na hasa ujenzi mpya kabisa," alisema.

Alisema ifikapo mwaka 2025 kila makao makuu ya tarafa itakuwa na majengo mapya ya mahakama.

Awali, Katika swali la msingi, Mbunge wa Hai (CCM), Saashisha Mafuwe, alihoji lini serikali itajenga majengo ya kisasa katika Mahakama ya Wilaya ya Hai kutokana na yanayotumika sasa kuwa chakavu.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Pinda alisema serikali ilikwishapeleka wataalamu na kubaini kuwa mahakama hiyo ni chakavu na ilihitaji ukarabati ambao tayari ulishafanyika tangu Februari, mwaka 2021.

## Walimu 1,000 kuajiriwa vyuo vya ufundi

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, imepanga kuajiri walimu wa vyuo vya ufundi 1,000 kupitia kibali kilichotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan hivi karibuni.

Naibu Waziri Omari Kipanga alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Nyasa (CCM), Stella Manyanya.

Katika swali lake, Mbunge huyo alisema tatizo linalokabili vyuo vya VETA ni upungufu mkubwa wa walimu na kuhoji serikali imejipangaje kuandaa walimu.

Kipanga akitoa majibu ya swali hilo, alisema kati ya ajira 2,035 zilizotolewa kibali na Rais Samia Suluhu Hassan hivi karibuni kwa wizara hiyo, ajira 1,000 ni za walimu wa vyuo vya ufundi.

Alisema hatua hiyo itapunguza upungufu wa walimu kwenye maeneo ambayo vimejengwa vyuo vipya.

Katika swali lingine la nyongeza, Mbunge wa Nanyamba (CCM), Abdallah Chikota, alihoji lini serikali itajenga Chuo cha VETA kwa ajili ya Wilaya ya Mtwara.

Kipanga alisema mkakati wa serikali kwa sasa ni kujenga kila wilaya nchini na baada ya hapo itafikiria kwenye wilaya zenye majimbo mengi ikiwamo Mtwara.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Muleba Kusini (CCM), Dk. Oscar Kikoyo, alihoji lini serikali itajenga Chuo cha VETA katika Wilaya ya Muleba.

Kipanga alijibu serikali inaendelea kujenga vyuo vya VETA katika mikoa na wilaya mbalimbali kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Alibainisha kuwa katika bajeti ya serikali mwaka ujao 2022/23, imetenga fedha kwa ajili ya vyuo 36 vya VETA kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Alisema katika kipindi ambacho serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha VETA katika Wilaya ya Muleba na maeneo mengine.

Pia, wananchi wa Muleba wanashauriwa kuendelea kutumia Kituo cha Ufundi Stadi katika wilaya hiyo (Ndolage VTC) pamoja na vyuo vya VETA na vyuo vya maendeleo ya wananchi vilivyoko kwa ajili ya kupata elimu na mafunzo ya ufundi.




Habari zote: Augusta Njoji DODOMA

Biashara 'online' inavyozidi kukua, wahusika wazisimamie wenyewe



Ukurasa 12

Nipashe
# TESA
Jumanne Juni 28, 2022
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 13

**Rushwa ya ngono vyuoni simu janja inavyoweza kuwakomesha wakware**

TEKNOLOJIA
NA GERALD KITABU

## UNAIJUA DHAHABU NYEUPE?

# Ni pamba inayolimwa karibu kila mkoa ndiyo mwajiri wa Watanzania mil.20

• Utafiti Ukiriguru unavyoboresha uzalishaji



Watafiti wa pamba wakiwa kazini kwenye mashamba ya wakulima. **PICHA: GERALD KITABU**

PAMBA ni zao linalotoa nyuzi asilia duniani kote, tena nyuzi hizo zina matumizi mengi ndiyo maana zipo jamii zinazoiita zao hilo "dhahabu nyeupe" kwa sababu ni ya thamani mno na inaendelea kubakia hivyo hata sasa.

Kwa Tanzania pamba ni muhimu kwa uchumi wa nchi na inashika nafasi ya nne kwa kuliingizia taifa fedha za kigeni.Haishii hapo, kilimo chake kinaajiri wakulima wadogo zaidi ya nusu 1,000,000, linalimwa karibu nchi nzima ndani ya mikoa 17 kati ya 26 ya Tanzania Bara.

Inalimwa na wakulima wadogo wenye wastani wa hekari moja kila mmoja na asilimia 99 ya pamba huzalishwa na wakulima hao, lakini hali ikoje kwenye utafiti wa uboreshaji pamba?

Nipashe inazungumza na Mratibu wa Utafiti Kitaifa wa zao hilo Dk. Paul Saidia, kutoka kituo cha utafiti wa kilimo TARI Ukiriguru kuhusu uzalishaji na changamoto ya zao hilo kwa sasa.

***SWALI:*** Mtafiti na mratibu wa pamba nchini, msomaji wa Nipashe angependa kujua taarifa za zao hili, idadi ya wakulima na manufaa yake kwa taifa na kimataifa.

***JIBU:*** Tukiangalia umuhimu, uzalishaji na maeneo yanayolimwa pamba nchini zao hili hulimwa na wakulima takribani 500,000 katika mikoa 17 na wilaya 56. Ukulima ukifanyika kwenye eneo la ekari takribani 1,000,000.

Kwa upande wa mnyororo wa thamani kwenye zao hili, zaidi ya asilimia 40 ya Watanzania hutegemea mnyororo wa thamani wa pamba.

Robota moja lenye kilo 227 huzalisha suruali 215 za jinzi, shuka 250 za kitanda cha futi tatu 750, mashati 1,200, fulana 3,000 nepi 4,300, soksi 2,100 na pamba za kuondolea uchafu masikioni 680,000. Tani ya mbegu inazalisha lita 200 za mafuta, kilo 500 za mashudu, pumba kilo 300 na lita 40 za magwanji ya kutengenezea sabuni.

***SWALI:***Watanzania wangependa kujua zao hili hulimwa wapi hapa nchini?

***JIBU:*** Inazalishwa kwenye mikoa ya kanda ya mashariki ambayo ni pamoja na Morogoro na Pwani kwa asilimia moja mpaka tatu, lakini hulimwa kanda ya magharibi na wakulima wa mikoa ya Geita, Mwanza, Simiyu, Shinyanga, Katavi na Rukwa.

Asilimia 70 hadi 80 huuzwa kama malighafi (bila kuchakatwa) nje na kuingiza wastani wa dola milioni 120 za Kimarekani kwa mwaka. Pamba inatumiwa na viwanda vya nguo.

***SWALI:*** Mtafiti na Mratibu wa pamba kitaifa, mnafanya nini ili kuongeza uzalishaji wa zao hili?

***JIBU:*** Utafiti wa pamba unafanyika katika Taasisi za TARI Ukiriguru mkoani Mwanza na TARI Ilonga mkoani Morogoro. Ukiriguru imepewa jukumu la kusimamia utafiti wa pamba kitaifa.

Kwa kushirikiana na wadau wengine imejikita kushughulikia changamoto za mbegu bora, wadudu na magonjwa, agronomia na rutuba ya udongo, ubora wa nyuzi na usambazaji wa teknolojia. Kadhalika taasisi hii inajishughulisha na mabadiliko ya tabianchi, uongezaji thamani ya pamba na masuala ya uchumi jamii.

***SWALI:*** Wakulima na Watanzania kwa ujumla wangependa kujua taarifa za mbegu bora za pamba.

***JIBU:*** Mbegu bora za pamba ni pamoja na hizi zilizopewa majina ya kitaalamu kama UKM 08, UK 173 na UK 171 kwa kanda ya magharibi. Lakini kuna NTA 93-2 na Mkombozi wa Kanda ya Mashariki. Japo kwa sasa mbegu ya UKM 08 ndiyo inatumika kama mbegu ya kibiashara Tanzania.

***SWALI:*** Kuna utafiti gani unaoendelea kuhusu mbegu bora za pamba?

***JIBU:*** TARI Ukiriguru inaendelea kutafiti mbegu bora. Sifa zinazoangaliwa ni pamoja na mavuno mengi, asilimia ya uchambuzi, ubora wa nyuzi, ukinzani dhidi ya ugonjwa wa mnyauko fusari na ukinzani dhidi ya wadudu waharibifu kama vile chawajani na visumbufu vingine. Kwa sasa ukinzani dhidi ya mdudu chawajani utapewa msukumo wa kipekee.

***SWALI:*** Vipi kuhusu wadudu na magonjwa yanayoshambulia pamba?

***JIBU:*** Wadudu wanaoibukia kuwa tishio ni pamoja na chawajani, vidung'ata na vithiripi, na viwavi jeshi vamizi. Pia ugonjwa wa mnyauko futhari unaendelea kusumbua baadhi ya maeneo.

***SWALI:*** Mnafanya jitihada gani kudhibiti wadudu hawa waharibifu na magonjwa haya?

***JIBU:*** Jitihada za TARI Ukiriguru kudhibiti magonjwa haya ni pamoja na kuweka mkakati wa muda mfupi mfano matumizi ya viuwadudu vyenye, uwezo wa kudhibiti. Huu ulifanyika kwenye wilaya nne msimu wa kiangazi 2019, katika Wilaya za Misungwi, Kwimba, Maswa na Meatu.

**INAENDELEA UK.12**

TEKNOLOJIA

NA NIMI MWETA

# Biashara ‘online’ inavyozidi kukua, wahusika wazisimamie wenyewe

WAKATI biashara ya kupeleka fedha kwa mtandao sasa imezoeleka, kutumia huduma hiyo kuuza bidhaa inaweze kukasuasua zaidi kutokana na kukosekana uaminifu kwa wahudumu wanaofikisha bidhaa kwa wateja.

Ni hali ambayo inajitokeza katika majadiliano ya hapa na pale kuhusu biashara mitandaoni, kwa kutumia kibwagizo cha ‘umepigwa,’ kwa maana ya kutoa fedha ili kupelekewa bidhaa, lakini baada ya kutuma fedha namba ya simu ya muuzaji haipatikani.

Inawezekana ni matapeli wachache wanaofanya hivyo, ila wanawastua wengi kwani hakuna anayejua ni wapi balaa hilo litatokea atume pesa halafu ‘mzigo’ usifike na hela zipotee.

Ukiangalia katika matangazo mfano kwenye Google unakutana na biashara ya bidhaa kuuzwa mtandaoni na kupelekewa kwa wateja mitaani.

Kukua kwa mfumo huo wa biashara ni moja ya sababu za jitihada ya kufanikisha mpango wa taifa wa anuani za makazi.

Mtu anajiunga na ukurasa wa ‘shopping mall’ au duka kubwa fulani au ‘supermarket,’ apige simu ipokelewe na mhudumu atoe oda ya mahitaji, apite katika shelifu za bidhaa ndani ya duka hilo, azichukue huku akimwangalia kutoka nyumbani kwake.

Bidhaa hizo baada ya kulipiwa zinapelekwa kwa mteja kwa gari la wakala wao anayefikisha bidhaa majumbani.

Ina maana kuwa kuuza bidhaa mtandanoni kunahitaji uwazi unaofanana na mteja kuingia dukani na kununua vitu, kwani mnunuzi anaona kila kitu kana kwamba ni yeye anayechagua.



Kuuza na kununua mitandaoni kunataka uaminifu ili kuwafikishia wateja bidhaa wanazonunua kwa wakati na kwa usahihi. **PICHA: MTANDAO**

> Matumizi ya Whatsap yanawaunganisha wateja, wajadili bei, walipe na kuhakikishiwa kupelekewa

Kwa hali hiyo kuna maeneo ambako biashara ya mitandaoni inafanya kazi vyema na ukitazama kinachotangazwa zaidi unakuta ni bidhaa za kielektroniki na nyinginezo za majumbani, na hasa za bei mbaya.

Kwa bidhaa kama hizo wanunuzi wake si ule umati unaopita barabarani kutafuta vitu vya bei nafuu ila watu wanaojiweza wasiotaka kusumbuliwa na kuendesha gari hadi dukani, au kupitia duka moja hadi jingine kuangalia bidhaa.

Waendeshaji wanatakiwa pia kuwa na kampuni ambazo zinajiweza, zinazotaka kila mteja anayepatikana atoe ushuhuda wa huduma nzuri na bidhaa bora, ili aendelee kuwa mteja wao.

Ndiyo hapo inakuja dhana kuwa kuwapo kwa biashara mtandaoni inatosha tu kuwa na duka au kituo cha huduma na kukitangaza, kwani wateja wengi wanafutatilia kurasa za Instagram au wanapachika huko uwepo wa bidhaa na vituo vyao.

Mchangiaji mmojawapo kuhusu upatikanaji wa bidhaa kwa mtandao hapa nchini anasema kuwa kuna vituo vingi vya mauzo vilivyoko mitandaoni ila ni vichache ambavyo vinapata biashara kwa wingi.

Matumizi ya Whatsap yanawaunganisha wateja, wajadili bei, walipe na kuhakikishiwa kupelekewa bidhaa kwa wanunuzi.

Hata hivyo mchangiaji mmoja anaeleza kuwa zaidi wateja wanapatikana kwa ushuhuda wa mtu mmoja mmoja anayemvutia mwingine kuingia au kutumia kituo hicho cha mauzo.

Na kwa vile siyo rahisi kusoma maelezo ya ‘waliopigwa’ katika mitandao ya jumla, nje ya akaunti au kurasa, inazohadithia masaibu binafsi, kujua hitilafu katika mpangilio huo inaweza kutokea wapi siyo rahisi, hivyo kwa haraka, ni kwa wauzaji matapeli wanaotumia mtandao na simu kwa njia ya kujificha.

Ni kudiriki kwa kiwango fulani kwani kimsingi inawezekena kumfuatilia mmiliki wa simu endapo ataitumia kufanya utapeli, ila ni usumbufu.

Biashara mitandaoni zinafana zaidi pale ambako kuna kampuni inayojulikana kwa watu wengi isiyotaka jina lake kuharibiwa kwa kushirikiana na madereva wasioaminika, wasiofikisha bidhaa walikoelekezwa.

Mmiliki wa biashara inayotumia mtandao kunadi bidhaa, kuuza na kuzipeleka kwa wateja anatakiwa kuwa mmiliki au msimamizi wa mtiririko wote huo.

Akihusisha watu wengine wanje ambao hawaogopi kuulizwa au kukemewa na mwenye biashara mtandaoni, atamharibia biashara kwa kukosa uaminifu na kumgombanisha na wateja.

Au mtu afungue kituo cha mauzo kwa nia njema halafu amwajiri ndugu au mtu mwingine mradi ana cheti katika uendeshaji wa biashara kama hiyo, halafu hafuatilii kwa karibu.

Endapo hayuko tayari kusimamia mwenyewe na kupokea malalamiko yanapotokea, anaweza kuhatarisha biashara, watu wakiambizana mitandaoni kilichotokea na matokeo yake ni kibwagizo cha ‘kupigwa.’

## Ni pamba inayolimwa karibu kila mkoa ndiyo mwajiri wa Watanzania

**INATOKA UK.11**

Maendeleo yalikuwa mazuri, pia tuna udhibiti wa muda mrefu ambao ni pamoja na udhibiti husishi, ukinzani wa mbegu kwa mdudu chawajani, kuendelea na utafiti wa viuwadudu vipya kufuata spraying regime na upuliziaji kufuata wingi wa wadudu shambani Economic thresholds.

Ugonjwa wa mnyauko fuzari unaendelea kufanyiwa utafiti wa kutambua kuenea kwake, mafunzo yataendelea kutolewa ya kuzuia kuenea kwa mnyauko fuzari kuanzia maeneo ya kupanda mbegu hadi shamba hadi shamba na mbegu zenye ukinzani zinaendelea kufanyiwa utafiti.

**SWALI:** Umetaja agronomia ya pamba. Hii ina kazi gani?

**JIBU:** Hii ina maana ya matumizi ya kanuni bora za kilimo cha pamba. TARI Ukiriguru inaendelea kuhimiza kanuni 10 za kilimo bora cha pamba hususan nafasi na mbolea. Mikoa wa Dodoma na Katavi nayo itapewa kipaumbele.

**SWALI:** Je, kuna utafiti wowote wa kiuchumi mnaofanya kuhusu zao hili?

**JIBU:** Ndiyo lengo ni kumwongezea mkulima uwezo wa kutambua kilimo biashara cha zao la pamba, kujua changamoto zilizoko katika mnyororo mzima wa thamani na kutoa mapendekezo stahiki.

Pia uongezaji thamani ya zao la pamba na utafiti nyuzi za pamba unaolenga kuongeza ubora wa pamba ili itoe nyuzi zitakazofaa kwa matumizi yanayokusudiwa.

Kulinda ubora wa pamba ya Tanzania pia mafunzo kuhusu umuhimu wa uchambuaji pamba mbegu kabla ya kuuzwa.

**SWALI:** Kama mtafiti na mratibu wa zao hili kitaifa tueleze kuhusu mwelekeo wa utafti wa pamba nchini.

**JIBU:** Tunamalizia utafiti wa mbegu ya pamba yenye kinzani dhidi ya mnyauko fusari na kuzitoa rasmi kutumika. Utafiti utafanyika wa kuongeza vinyweleo kwenye pamba ili iwe na ukinzani wa kutosha dhidi ya chawajani na wadudu wengine wafyonzao. Utafiti wa viuwadudu sumu vyenye uwezo mkubwa wa kudhibiti chawajani, vithiripi, vidung’ata na viwavijeshi vamizi. Tunayo pia mikakati ya utafiti wa pamba kuongeza nguvu zaidi kama vile udhibiti husishi wa wadudu hao.

ELIMU
NA SABATO
KASIKA

# Rushwa ya ngono vyuoni simu janja inavyoweza kuwakomesha wakware

• Ni rahisi waathirika kufunguka kupitia mitandao

SIYO siri wasichana wengi wanafahamu kuwa wanapoelekea kujiunga na chuo kikuu kuna kigingi kinachowasubiri pale watakapoingia chuoni, lipo shinikizo la kufanya ngono ili kupata alama za juu au kufaulu. Hata hivyo, wanasikia kuwa pale unapokuwa jasiri na kukataa tena ukaripoti kwa mamlaka za chuo mara nyingi haki huwa ngumu kupatikana.

Ndiyo maana rushwa ya ngono kwa wanachuo wanawake walio kwenye taasisi za elimu ya juu inaweza kufananishwa na ugonjwa sugu unaowatafuna na kuwavuruga wasomi hao kiafya, kitaaluma na hata kuyumbisha hatima za baadhi.

Maradhi hayo wakati yakiendelea kuumiza wengi, wasichana wanadaiwa kupata 'shahada za ngono'. Ni kwa sababu hawajisomei kikamilifu ili kupata 'digrii' badala yake miili yao ndiyo inayowapa alama au maksi za juu kwenye mitihani, au wakati mwingine wahadhiri na maprofesa wanawafanyia mitihani kwa malipo ya ngono.

Taasisi ya Ustawi wa Jamii Dar es Salaam, imekuna kichwa kwa miaka mitatu na sasa imekuja na njia inayoweza kusaidia kutatua tatizo hilo, ufumbuzi unaokuja baada ya kufanya utafiti.

Taasisi hiyo imebaini kuwa, mitandao ya kijamii ikiwamo ya Facebook, Twitter na Instagram inaweza kusaidia kukabiliana na ukatili wa rushwa ya ngono vyuoni.

Mmoja wa wahadhiri wa taasisi hiyo, Dk. William Manyama, anasema mitandao hiyo inaweza kuwa na matokeo chanya iwapo itatumika inavyotakiwa.

Anaeleza kuwa mitandao ya kijamii inasaidia kukabiliana na ukatili wa kingono kwa sababu; inawapa nguvu watumiaji kutoa taarifa, mitandaoni watu wanaweza kufunguka kwa urahisi na wepesi kuliko kutumia utaratibu wa uso kwa uso.

Ni rahisi kuitumia kwa vile mhusika anaweza kurekodi sauti na kueleza kisa chote, mazingira ya udanganyifu, mbinu chafu na kutaja hata majina ya watuhumiwa kuliko kama ingekuwa ni mazungumzo ya ana kwa ana.

Mbali na hayo ikitumiwa ipasavyo inaweza kuharibu mtandao wa desturi potofu na kuvunja ukimya kwa vile inazizungumzia, ikiziibua taarifa zake hufika kwa wadau ikiwamo serikali lakini huamisha watu kuzijua na kuzikataa.




Dk. William Manyama akiwasilisha ripoti ya utafiti huo. **PICHA: MARCO MADUHU**

Utafiti unaonyesha kuwa, pamoja na kuwapo na changamoto, mkitandao ya kijamii ina mchango mkubwa kukabiliana na ukatili wa kingono.

Anasema hayo wakati akielezea utafiti wao waliofanya kwa miezi mitatu kuanzia Julai hadi Oktoba mwaka jana kuona jinsi mitandao inavyoweza kutumika kumaliza tatizo hilo.

Dk. Manyama anatoa ripoti ya utafiti huo kwa wanahabari jijini Dar es Salaam wiki iliyopita na kuelezea jinsi walivyofanya utafiti huo uliohusisha makundi mbalimbali ambao ulifanyika katika mitandao ya Facebook, Instagram, Twitter, ticktack na What's app.

"Tulitaka kupata suluhu kutokana na madhara ambayo yamekuwa yakisababishwa na rushwa ya ngono kwa wanafunzi vyuoni na kujua aina ya mitandao inayotumika, tulifuata mitazamo ya wanafunzi kuhusu mitandao na pia tulichunguza vikwazo wanavyopata ili waweze kukabiliana na vitendo vya ukatili," anasema Dk. Manyama.

### MBINU ZILIZOTUMIKA

Mhadhiri huyo anataja mbinu waliyotumia kuwa ni kuhoji mtu mmoja mmoja na makundi mawili ya wanawake na wanaume ambayo hayakuzidi watu 12.

"Mahojiano yalikuwa ya kina tulianzia kwa wanafunzi 14 wa Taasisi ya Ustawi wa Jamii Dar es Salaam na Kisangara wilayani Mwanga mkoa wa Kilimanjaro," anasema.

Anafafanua kuwa, matokeo ya utafiti huo yalibaini kuwa mitandao inapendwa kwa sababu ya ushirikiano wa watu wengi, wanafunzi wana uelewa mkubwa wa mitandao hiyo na haiepukiki, na kwamba elimu itolewe kuhusu matumizi bora, inaweza kupambana na ukatili wa rushwa ya ngono.

### INAVYOMALIZA TATIZO

Manyama akielezea jinsi walivyobaini mitazamo chanya na hasi, anasema kwa upande wa chanya, mitandao inasaidia kupashana habari kwa kuwa wakati watu hawawezi kukutana uso kwa uso na inatoa taarifa, kupata ushauri na inakuwa rahisi kupata msaada baada ya tatizo kuwafikia wengi zikiwamo mamlaka zenye uwezo wa kudhibiti.

> Mahojiano yalikuwa ya kina tulianzia kwa wanafunzi 14 wa Taasisi ya Ustawi wa Jamii Dar es Salaam na Kisangara wilayani Mwanga mkoa wa Kilimanjaro

"Iwapo mtu akitumia vizuri mitandao, anaweza kuwa salama, kwani ni rahisi kujisajili, lakini kwa upande wa mtazamo hasi, wengine wanasema mitandao inachangia kufanya ukatili uendelee hasa pale inapotumika vibaya, kwani wapo wanatoa taarifa na kudharauliwa," anasema.

Anasema, pamoja na kuwapo kwa hoja hizo kinzani, watafiti hao wanahitimisha kuwa mitandao ya kijamii ina nafasi kubwa ya kusaidia kukabiliana na ukatili wa rushwa ya ngono, kwa kuwa hiyo ndiyo hoja yenye nguvu.

### VIKWAZO NJIANI

Aidha, Dk. Manyama anaongeza kuwa, katika utafiti wao, wamebaini changamoto ambazo ni ukosefu wa fedha za kujiunga na vifurushi na kutoa taarifa na kuzomewa.

"Lakini utafiti ulilenga kupanua mawazo na jinsi ya kukabiliana na ukatili wa kingono, ambapo elimu ni ya muhimu, kwani bado kuna changamoto ya kujua cha kuweka katika mitandao, watu gani na wakati gani, ili wanafunzi watumie vizuri mitandao ya kijamii kwa ajili kuwapatia haraka suluhu," anasema.

Naibu Makamu Mkuu wa taasisi hiyo, Profesa Justine Urassa, anawashauri walimu na wanafunzi kufanya utafiti na kwamba taasisi itawawezesha.

"Utafiti wa mtandao una manufaa mengi, kwani vitendo vya ukatili wa rushwa ya ngono vipo ndani ya jamii yetu. Lakini utasaidia vyombo vya dola kubaini namna ya kupambana navyo," Prof. Urassa anasema.

Anaeleza kuwa mwanafunzi anapokuwa chuoni, anatakiwa kusoma bila kubughudhiwa, na kwamba atasaidia wenzake kujua jinsi ya kukabiliana na ukatili na namna ya kupata ushauri sahihi kwa kuwa wakati mwingine mitandao inatumika kuchochea ukatili, hivyo wanataka namna nzuri ya kunitumia.

Prof. Urassa anasema, kupitia mitandao wanafunzi wanaweza kukutana na wataalmu sahihi ili kupata ushauri bora na msaada mwingine na kwamba wataende-

INAENDELEA UK.14

# Rushwa ya ngono vyuoni simu janja inavyoweza kuwakomesha wakware



Baadhi ya wadau wakifuatilia uwasilishaji wa ripoti hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**INATOKA UK.11**

lea kufanya utafiti kwa kuwa jamii inabadilika, hivyo ni muhimu kuja na njia nzuri ya kwenda na wakati ukatili wa aina yoyote katika jamii.

**CHANZO CHA RUSHWA**

Utafiti wa rushwa ya ngono vyuoni uliofanywa na Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa (TAKUKURU) mwaka 2020 unabaini chanzo cha rushwa hiyo kuwa baadhi ya wahadhiri wa vyuo kutumia mamlaka yao kushawishi ngono.

Ripoti ya utafiti huo inaonyesha kuwa wanafanya ushawishi wa rushwa ya ngono kwa wasichana kwa lengo la kuwapa viwango vya juu vya ufaulu kwa kuwapa alama kubwa zisizoendana na uwezo wao.

Ukifanyika katika vyuo vikuu vya Dodoma (UDOM) na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), unabaini kuwa asilimia 50 ina uelewa wa rushwa ya ngono na kwamba baadhi ya wasichana ambao hukataa kutoa rushwa ya ngono wamekuwa wakipata wakati mgumu katika masomo yao.

Mwendesha mashtaka wa TAKUKURU, Denis Lekayo, ndiye anayesoma ripoti ya utafiti huo mbele ya wadau wa kupambana na rushwa hiyo jijini Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa Lekayo katika utafiti huo watu 589, wanafunzi wa UDSM wakiwa 352 na 237 wa UDOM mbinu za uchunguzi zilitumika kwa lengo la kupata taarifa za kina namna rushwa ya ngono kwa wasichana wa vyuo inavyotendeka.

Matokeo yakabainisha kuwa wanafunzi asilimia 81.6 waliohojiwa na watumishi 91.4 walikuwa na uelewa wa dhana ya rushwa ya ngono. Mwendesha mashtaka huyo anasema, zaidi ya asilimia 50 ya waliohojiwa walieleza uwapo wa rushwa ya ngono katika vyuo vikuu vilivyofanyiwa utafiti na kufanya suala hilo kunamaanisha kwamba rushwa ya ngono ni tatizo katika vyuo vikuu hivyo.

Lakini akabainisha kuwa utafiti huo ulitaka kujua sababu zinazochochea rushwa ya ngono katika vyuo vikuu kwa kuwataja wahojiwa kueleza chanzo cha kuwapo vitendo vya rushwa ya ngono.

Akafafanua kuwa matokeo ya utafiti katika vyuo vyote viwili yamebainisha kuwapo kwa sababu tano ambazo ni ukosefu wa maadili, ushawishi wa mtu mwenye mamlaka, mfumo wa utoaji taarifa kutokuwa rafiki, mifumo dhaifu ya kushughulika na rushwa ya ngono na mamlaka ya kutoa alama za mitihani kuachwa kwa wahadhiri pekee.

Changamoto nyingine anayoitaja Lekayo katika utafiti huo ni matumizi mabaya ya madaraka ya kujinufaisha kingono kwa kutoa alama ambazo haziendani na mfanyiwa ngono, uadilifu mdogo, uongozi na kamati za maadili kutokuwa na maadili na wakati mwingine kamati hizo kufanya vitu ambavyo vinawafanya watu wasiwaamini.

Lakini, akifafanua kuwa mhadhiri ana ushawishi mkubwa katika kutenda vitendo vya rushwa ya ngono, mara nyingi malalamiko yanayopelekwa na hayashughulikiwi kutokana mhadhiri kuwa sehemu ya ngono hizo na mamlaka za vyuo vikuu kulindana na kuteteana.

## WANENAVYO MALENGA

### MAWIGI KUAZIMANA

Mawigi kuazimana, kumeshamiri kwa sana,
Jinsi watu wapeana, hakuna kuulizana,
Wanawake twawaona, kupendeza washindana,
Biashara hii nzuri, lakini ina madhara.

Nywele za bandia sana, watu wengi twawaona,
Mwonekano bora sana, njiani tukipishana,
Kununua wanaona, wanajisumbua sana,
Biashara hii nzuri, lakini ina madhara.
Siyo pesa nyingi sana, jinsi wanaazimana,
Kwa siku moja peana, buku tano taziona,
Kwa wiki watu wavuna, mifuko yao hutuna,
Biashara hii nzuri, lakini ina madhara.

Magonjwa ambukizana, hayo twaweza yaona,
Mba fangasi kiona, usije shangaa sana,
Wigi kubadilishana, inasababisha sana,
Biashara hii nzuri, lakini ina madhara.

Urembo mzuri sana, watu wapendeza sana,
Lakini ni ghali sana, tusije kudanganyana,
Kama wautaka sana, nawe gharamika sana,
Biashara nzuri sana, lakini ina madhara.

Mawigi kuvaliana, na nguo kuazimana,
Hiyo ni hatari sana, yale utayokumbana,
Utashangaa kuona, hata chawa wengi sana,
Biashara hii nzuri, lakini ina madhara.

Afya ni muhimu sana, sote tunahimizana,
Wigi si muhimu sana, hasa la kuazimana,
Magonjwa ambukizana, sawa na kuzuliana,
Biashara hii nzuri, lakini ina madhara.

Mawigi wapenda sana, yanunue mengi sana,
Mambo ya kungojeana, mpate kuazimana,
Hayo ni mabaya sana, hatari mbele twaona,
Biashara hii nzuri, lakini ina madhara.

Mawigi kukodishana, pesa nyingi kuziona,
Hasara bora kuona, tusijekumalizana,
Bora vingine kuona, si vema kuazimana,
Biashara hii nzuri, lakini ina madhara.

Wigi kuazimana, na watu kuchangamana,
Familia utaona, nayo mwaambukizana,
Shida hiyo kubwa sana, acheni kuazimana,
Biashara hii nzuri, lakini ina madhara.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**

### PATRICE LUMUMBA: NI SHUJAA WA AFRIKA

Imetokea habari, jamaa wameandika,
Ya kiongozi mahiri, ambaye twamkumbuka,
Maarufu na jasiri, hapa kwetu Afrika,
Japo limebaki jino, ni shujaa wa Afrika.

Ni Patrice Lumumba, vibaya aliondoka,
Risasi walimlamba, ila hawakutosheka,
Kaburi wakalichimba, ili aweze futika,
Japo limebaki jino, ni shujaa wa Afrika.

Likatwakatwa vipande, aweze kumalizika,
Na hata vile vipande, bado hawakutosheka,
Hofu wao iwapande, tusije kumkumbuka,
Japo limebaki jino, ni shujaa wa Afrika.

Kwenye ile tindikali, mwili wakauchomeka,
Uliteketea kweli, lakini hajafutika,
Kwenye moyo na akili, Lumumba twamkumbuka,
Japo limebaki jino, ni shujaa wa Afrika.

Bingwa Patrice Lumumba, Kinshasa kwao hakika,
Kupambana hakuyumba, kusema Wazungu toka,
Jinsi alivyowachimba, na wao wakageuka,
Japo limebaki jino, ni shujaa wa Afrika.

Mpigania uhuru, sisi tunamkumbuka,
Kwa ukombozi ni nuru, ukoloni kutoweka,
Kweli tunamshukuru, japo alishatoweka,
Japo limebaki jino, ni shujaa wa Afrika.

Jino limepatikana, habari imetamka,
Mtu amepatikana, kumuua mhusika,
Jino lake liliona, na hilo akaondoka,
Japo limebaki jino, ni shujaa wa Afrika.

Hivi DR ya Congo, ni nani anayefika,
Ambaye kwetu kigongo, mashujaa kufunika?
Bila kusema uongo, Lumumba anafunika,
Japo limebaki jino, ni shujaa wa Afrika.

Jino limepatikana, twazidi kumkumbuka,
Kabla ya kuliona, Lumumba twamkumbuka,
Mitaa utaiona, na majina yatumika,
Japo limebaki jino, ni shujaa wa Afrika.

Afrika twamuenzi, kwa kazi njema hakika,
Kwa majina na utunzi, kazi aliyoishika,
Alikuwa ni kurunzi, Afrika kukomboka,
Japo limebaki jino, ni shujaa wa Afrika.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**



## Injini 320 kununuliwa kuimarisha sekta uvuvi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amesema serikali imejipanga kununua injini 320 za boti katika mwaka wa fedha wa 2022/23 ili kuimarisha sekta ya uvuvi nchini.

Ndaki alisema hayo jana alipokuwa akikabidhi injini za boti kwa ajili ya wavuvi katika Halmashauri za Wilaya za Pangani, Mtwara Mjini na Iringa.

Alisema lengo ni kuhakikisha uzalishaji wa mazao ya uvuvi unaongezeka na mchango wake katika kukuza kipato cha mvuvi na taifa kwa ujumla.

"Kwa kufanya hivyo lengo la Rais Samia Suluhu Hassan litakuwa limetimia kwa kuhakikisha kipato cha wavuvi kinaongezeka na mchango wa uvuvi kwenye pato la taifa unaongezeka," alisema.

Vilevile, Waziri Ndaki, alisema kuwa injini hizo zitatolewa kwenye vyama vya ushiriki vya wavuvi na kwa mvuvi mmoja mmoja mwenye uwezo na zitakuwa zikikopeshwa kwa riba ndogo.

Alisema wizara imeendelea na utaratibu wake wa kuwawezesha wavuvi kwa kuwapatia vifaa vitakavyowasaidia kuongeza uwezo wa kuvua mazao ya uvuvi kwa wingi.

"Injini za boti tunazozikabidhi leo zina uwezo wa nguvu ya farasi 15 na tunazitoa kwenye Halmashauri za Wilaya za Pangani, Mtwara Mjini na Iringa ambapo kila halmashauri itapata injini moja kwa ajili ya kuwawezesha wavuvi kuongeza uwezo wao wa kuvua pia kulinda rasilimali za uvuvi," alisema.

Naye Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, ambaye ni Mbunge wa Pangani, alishukuru wizara kwa kuwapatia injini hiyo ambayo itakuwa msaada mkubwa kwa wavuvi na ulinzi wa rasilimali za uvuvi.

Mbunge wa Mtwara Mjini, Hassan Mtenga, aliomba wizara kuendelea kuwawezesha wavuvi kwenye vifaa vingine vya uvuvi ikiwamo majokofu ya kuhifadhia mazao ya uvuvi.

Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Sekta ya Uvuvi, Dk. Nazael Madala, alisema wizara ina utaratibu wa kuwawezesha wavuvi kwa kuwapatia vifaa mbalimbali vinavyowasaidia kuongeza uwezo wao wa kuvua mazao hayo kwa wingi zaidi.

# ACVF yazindua kampeni kupinga rushwa nchini

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

TAASISI ya Sauti za Wapinga Rushwa (ACVF), imezindua kampeni ya 'badili tabia sepesha rushwa' itakayotekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu katika mikoa ya Dodoma, Dar es Salaam na Arusha ili kusaidia harakati za kuzuia vitendo vya rushwa nchini. Kampeni hiyo inahusisha mabalozi 365 waliopatiwa mafunzo na Taasisi ya Kupinga na Kupamba na Rushwa nchini (TAKUKURU).

Akizungumza kwenye uzinduzi huo jana jijini hapo, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, aliitaka taasisi hiyo kufanya kazi kwa malengo yaliyokusudiwa ili kukomesha vitendo vya rushwa nchini.

Aidha, Mtaka aliwahakikishia mabalozi wa kupinga rushwa kuwa atawapa ushirikiano ili kuhakikisha wanafanikisha kampeni hiyo ikiwa ni pamoja na kuandaa mkutano mkubwa wa wadau wote wakupinga rushwa.

"Nimefurahi mno kuona kuna watu bado hawalali wanaendeleza mapambano ya rushwa, nani asiyependa kuona rushwa inatokomezwa, ninawaahidi kwa nafasi yangu nitafanya mkutano mkubwa na kuwashirikisha klabu zote za wapinga rushwa wote wa shule ya msingi hadi vyuoni hii itasaidia kutengeneza mabalozi wa rushwa kwa kila maeneo ambayo serikali imepeleka fedha za miradi," alisema.

Alisema nia ya serikali kuona kunakuwa na mabalozi wapinga rushwa hadi vyuoni na wanafunzi wengi wanalalamika mambo hayako sawa kutokana na rushwa ya ngono.

"Tunaposepesha rushwa lazima tuone umuhimu wa kuingia kiundani zaidi ili tusepeshe kiukweli tusipoongeza juhudi hata watoto wetu wanaofanyiwa ukatili wa kingono mashuleni wakija kuajiriwa nao wanaweza kurithi vitendo hivyo na kuwafanyia wengine kama malipizi, niwahakikishie kwa hili mimi nitakuwa championi," alisisitiza.

Naibu Mkuu wa TAKUKURU, Mkoa wa Dodoma, Victor Swella, alisema ofisi hiyo itashirikiana na ACVF kutoa elimu kwenye makundi mbalimbali kwenye mapambano ya rushwa.

Alisema lazima kuwe na mipango mizuri ya kuratibu namna ya kutoa elimu ili kuwafikia watu wote kwa urahisi ikiwa ni pamoja na kuwafuata wananchi kwenye mitaa na maeneo yao ya kazi.

"Tupeleke zaidi elimu kwa watu wa chini ambao wananyimwa haki yao kwa sababu ya rushwa kuna wengine hata hawajui viashiria vya rushwa ni kazi yetu kuelimisha bila kuchoka ili kila mtu aishi kwa amani na utulivu," alisisitiza.

Katibu Mtendaji wa Mabalozi wa Sauti ya wapinga rushwa (ACVF), Kubega Dominick, alisema kampeni hiyo tayari imezinduliwa jijini Dar es Salaam na hivi karibuni itazinduliwa Jiji la Mwanza.



Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri (kulia), akinywa uji uliotengenezwa na unga wa ubuyu kutoka kwa mmoja wa wajasiriamali alipotembelea banda lake juzi kwenye hafla ya kukabidhi hundi ya Sh. bilioni 1.512 kwa vikundi vya wanawake, watu wenye ulemavu na vijana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Taasisi kilimo zaagizwa kupima afya udongo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WIZARA ya Kilimo imezielekeza taasisi zake kupita kwenye kanda za ikolojia nchini na kupima afya ya udongo, ili mbolea itakayozalishwa kwenye Kiwanda cha Itracom iendane na mahitaji ya udongo wa eneo husika.

Taasisi hizo ni ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea nchini (TFRA).

Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki katika ziara ya wabunge wa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini walipotembelea kiwanda hicho kinachotarajiwa kuanza uzalishaji mwezi ujao.

Alibainisha kuwa sababu kubwa ya kufanya hivyo ni pamoja na kutaka kujua aina ya udongo uliopo katika maeneo tofauti nchini, ili mbolea hiyo inapoanza kusambazwa iende kuleta mafanikio kwa wakulima nchini kwenye mazao wanayolima.

"Kabla ya kuanza uzalishaji tayari serikali ilishatoa maelekezo kwa taasisi zake husika kwenda kufanya tafiti, ikiwamo kuangalia aina ya udongo katika mikoa mbalimbali hapa nchini na kubaini mbolea aina ya Organo Mineral inayotarajia kuzalishwa kiwandani hapo ina tija," alisema Mavunde.

Alisema serikali inatambua Nyanda za Juu Kusini ni eneo la kiikolojia ambalo linategemewa sana kwa ajili ya uzalishaji wa mazao ya kilimo ndiyo maana wabunge wa maeneo hayo wafike kiwandani hapo kuona uzalishaji wa mbolea.

Mavunde alisema uwekezaji wa kiwanda hicho ni matunda ya ziara ya Rais Saia Suluhu Hassan na kumkaribisha mwekezaji kuja kuwekeza katika eneo hilo.

Hata hivyo, alisema baada ya kupanda kwa bei ya mbolea, serikali imekuja na mkakati tofauti wa kukabiliana na tatizo hilo na mkakati wa kwanza wa haraka ilikuwa ni kushirikisha TFRA kuhakikisha inatoa bei elekezi ili mbolea isipande bei kwa maeneo ambayo gharama yake halisi aiendani na uhalisia.

Alisema TFRA walianza kutoa bei elekezi na ilikuwa kama hatua ya muda mfupi, hatua ya muda wa kati ilikuwa katika bajeti mpya ya serikali inayoanza Julai mwaka huu, serikali imedhamiria kutenga fedha kwa ajili ya ruzuku ili kupunguza makali ya bei ambayo wananchi wanapata hivi sasa.

Mavunde alisema hatua ya tatu kama sehemu ya mkakati ilikuwa ni kuvutia wawekezaji kuja kujenga viwanda vingi nchini, mojawapo ni kiwanda hicho cha Itracom ambacho kina uwezo wa kuzalisha tani 600,000 kwa mwaka.

Alisema hivi sasa mahitaji ya samadi katika hatua ya awali ni tani 117,000, tayari wameshatengeneza vituo vya kukusanyia samadi hiyo na wafugaji watapata fursa ya kujipatia kipato kupitia mbolea inayozalishwa kiwandani hapo.

Naye mwenyekiti wa muda wa wabunge hao, Jackson Kiswaga, aliishukuru serikali kutokana na uwekezaji wa kiwanda hicho waliofanya nchini.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa kiwanda hicho, Nduwimana Nazaire, aliahidi hawataiangusha serikali na mbolea wanayokwenda kuzalisha italeta matokeo chanya.





# Gereza kuhamishwa kupisha uchimbaji madini

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

KAMPUNI ya Panda Hill Tanzania Limited, imetenga Sh. bilioni 14 kwa ajili ya kuhamisha Gereza la Kilimo la Songwe ili kupisha uchimbaji wa madini aina ya Niobium yaliyogundulika mahali lilipo gereza hilo.

Akizungumza juzi kwenye kongamano la nishati na madini mkoani hapo, Mwakilishi wa Kampuni ya Panda Hill Tanzania Limited, Emmanuel Kisasi, alisema fedha hizo zimeandaliwa na zitaanza kutumika baada ya kumaliza mazungumzo na serikali.

Kadhalika, makazi 120 na wafungwa zaidi ya 600 wataondolewa na kujengewa miundombinu muhimu ikiwamo shule, misikiti, viwanja vya michezo, makanisa na umeme.

Emmanuel alitaja faida za madini hayo kuwa ni pamoja na kutengenezea injini za ndege, magari na ujenzi wa miundombinu ya madaraja ya miradi mikubwa likiwapo la Magufuli, Kigamboni na Tanzanite.

Faida nyingine za madini hayo ni kutengeneza mabomba ya mafuta na gesi, utengenezaji wa magari, marumaru za reli pamoja na kukata vyuma kwenye visima.

"Madini haya yana umuhimu mkubwa sana kwa uchumi wa nchi tumejipanga madini hayo yachakatwe nchini na kiwanda kitajengwa wilayani Mbeya katika Kijiji cha Songwe na baada ya kuchakatwa yatauzwa nje ya nchi," alisema Kisasi.

Alifafanua kuwa asilimia 54 za malighafi katika mradi huo zitachukuliwa kutoka nchini huku mirabaha na kodi itasaidia kujenga miundombinu mbalimbali kama barabara, madaraja na shule.

Akizungumzia mchakato wa kuhamisha gereza hilo, Mkuu wa Magereza Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Magereza ACP, Adriano Mduda, alisema mazungumzo bado yanaendelea ya uhamishaji wa gereza hilo na baada ya kukamilika watapewa taarifa.

Alisema kwa sasa hana taarifa ya lini gereza hilo litahamishwa licha ya kuwa Kampuni ya Panda Hill ilitangaza nia ya kuwekeza katika eneo hilo ili kufanya shughuli za uchimbaji wa madini ya Niobium ambayo yamegundulika kwenye kipande cha eneo lilipo gereza.

Alisema serikali ikitoa tamko la kuhamisha gereza hilo wapo tayari na kwamba madini hayo yamegundulika yalipo majengo ya gereza pekee, shughuli nyingine za kilimo zitaendelea kama kawaida baada ya taratibu zote kukamilika.

Akifungua kongamano hilo kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Simon Mayeka, alisema serikali imejipanga kuwawezesha wachimbaji wadogo kupata mikopo ya vifaa ili kurahisisha shughuli zao.

Alisema, kongamano hilo linawakutanisha wadau mbalimbali wa sekta ya madini kujadili kwa pamoja vikwazo na mikakati ya pamoja ili kila mmoja anufaike na sekta hiyo na kumwezesha kuongeza kipato kwenye familia yake na taifa pia.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, akipokea maelezo kwa fundi sanifu migodi kutoka Tume ya Madini, Ofisi ya Madini Mkazi mkoani Mbeya namna wanavyopima asilimia za madini ya metali kwenye sampo, wakati wa maonyesho ya kongamano la nishati na madini jijini humo jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## Polisi yawatia mbaroni watuhumiwa wizi wa kuvunja

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, limewakamata watuhumiwa wawili kwa madai ya kuvunja na kuiba mchana kwenye nyumba za watu baada ya kufanya msako mkali kwenye maeneo mbalimbali ya jiji hilo.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, watuhumiwa hao walikamatwa Juni 19 majira ya saa saba mchana katika eneo la Ilolo Kata ya Kiwira, wilayani Rungwe baada ya kupata taarifa kutoka kwa Hedson Kamage, aliyetoa taarifa Polisi ya kuibiwa runinga.

Baada ya taarifa hiyo Polisi walianza msako wa kuwatafuta waliohusika na wizi huo na Juni 21, majira ya saa sita mchana walimtia nguvuni Asajile Mwakyusa (20) mkazi wa Simike, jijini Mbeya akiwa na mali mbalimbali za wizi.

Kamanda Matei alisema Mwakyusa alikamatwa akiwa na runinga mali ya Kamage yenye thamani ya Sh. 260,000.

Mtuhumiwa mwingine, Boniphace Mwanjuguju (26), mkazi wa Isumba, wilayani Rungwe alikamatwa na Polisi akiwa na runinga yenye thamani ya Sh. 880,000.

Mwanjuguju alikamatwa Juni 20, majira ya saa saba usiku baada ya kupata taarifa kutoka kwa wasamaria wema kuhusu mtuhumiwa huo ambaye aliiba mali ya Juma Kalongo.

Katika taarifa yake Kamanda Matei alitoa wito kwa wazazi pamoja na walezi kuwa makini nyakati za mchana kwa kuwa watu wengi wanakuwa kazini.

Alisema Jeshi la Polisi limeweka mikakati kudhibiti vitendo vya wizi na kuwasihi wananchi kutoa taarifa za uwapo wa kundi la wahalifu katika maeneo yao.

**Kamanda Matei alisema Mwakyusa alikamatwa akiwa na runinga mali ya Kamage yenye thamani ya Sh. 260,000.**

# Wachimbaji wadogo wahamasishwa kujisajili TIC

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WACHIMBAJI wadogo wa madini kutoka mikoa ya Nyanda za Juu Kusini wameshauriwa kuongeza nguvu ya mitaji ili waweze kusajiliwa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na kupewa leseni kubwa za uchimbaji.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Meneja wa TIC, Kanda, Venance Mashiba, alipozungumza na Nipashe kuhusu mikakati inayofanywa na kituo hicho kuwawezesha wachimbaji wadogo wanufaike na fursa zilizoko kwenye kituo hicho.

Alisema TIC inaendelea kuwahamasisha wachimbaji wadogo kutafuta mitaji mikubwa ili kupata sifa ya kusajiliwa kuwa wafanyabiashara wakubwa kama sharti la kituo hicho kunufaika na fursa mbalimbali ikiwamo punguzo la gharama za uagizwaji wa vifaa vinavyohitajika kwenye shughuli za uchimbaji wa madini.

"Mchimbaji mdogo wa madini hawezi kunufaika moja kwa moja na fursa zilizoko ndani ya TIC hadi hapo atapokuza biashara yake na kuwa mchimbaji mkubwa, yapo mambo mengi ambayo tunayasimamia kwa mchimbaji mkubwa kama vile kusimamia shughuli zake za vibali na usajili ndani ya muda mfupi pamoja na kupata punguzo la asilimia kwenye vifaa atakavyoagiza nje ya nchi," alisema Mashiba.

Alisisitiza kuwa TIC inaendelea kuwahamasisha wachimbaji wadogo kujiunga kwenye kituo hicho ili kunufaika na fursa mbalimbali zilizoko kwenye sekta ya madini kama vile masoko na unafuu wa uendeshaji shughuli hizo.

Baadhi ya wadau wa sekta ya madini wamesema wachimbaji wadogo wanafanya kazi kwenye mazingira magumu ikiwamo tozo kutoka mashirika na taasisi mbalimbali na kusababisha wasipate faida kwenye shughuli zao.

Amos Abraham, mchimbaji mdogo wa madini wilayani Chunya, alisema endapo serikali itaondoa baadhi ya tozo itawasaidia kupata faida.

Alitoa kilio kingine cha wachimbaji hao kuiomba serikali kuwajengea kituo kitakacho wasaidia kupimiwa maeneo yote yenye madini.

Alisema kwa kufanya hivyo itasaidia kurahisisha shughuli za upatikanaji na uchimbaji wa madini na kuokoa uharibifu wa mazingira unaojitokeza wakati wa kutafuta madini ya dhahabu wilayani humo.



## Mradi umeme wa jua tegemeo visiwani

Na Mwandishi Wetu

SHIRIKA la Umeme Zanzibar (ZECO), limesema baada ya kumalizika kwa kazi ya uwekaji wa umeme wa jua katika kisiwa cha Njao na Kokota, sasa ni zamu ya mradi mkubwa wa nishati hiyo kuzalisha megawati 18 visiwani humo.

Mradi huo wa umeme wa jua unatarajiwa kukamilika mwaka 2025 na kupunguza tatizo la upungufu na ukosefu wa nishati hiyo.

Hayo yalielezwa na Mjumbe wa Bodi ya wakurugenzi ya shirika la Umeme zanzibar (ZECO) Azizi Said Ali, wakati akizungumza na wandishi wa habari baada ya kumaliza ziara ya bodi hiyo, kutembelea miradi ya umeme wa jua kisiwa cha Kokota na Njao.

Alisema miradi ya visiwa ni uwekejazi mkubwa ambao umefanywa na ZECO ili kufikisha nishati hiyo kwenye maeneo ambayo umeme wa gridi hauwezi kufika.

Aidha, alisema miradi hiyo imegharimu Dola za Kimarekani 400,000, huku akiwataka wananchi kuitumia fursa hiyo kwa kuunga umeme ndani ya nyumba zao.

"Tunapaswa kuishukuru serikali kwa kufanikisha juhudi mbalimbali, ZECO inaweweza nguvu kuhakikisha wananchi wote wananufaika kupitia umeme wa jua," alisema.

Meneja Mkuu wa ZECO, Mshenga Haidar Mshenga, alisema umeme wa nishati ya jua hauna tofauti na umeme wa gridi na kuwasihi wananchi wasiogope kuutumia.

Akizungumzia mikakati ya shirika, alisema ni kuwaungia umeme bure wananchi wa visiwa hivyo.

"Umeme mwingi unaozalishwa na matumizi bado ni madogo, ili mradi uweze kutikisika basi hata wananchi wote wakaungiwa huduma hiyo, itakua bado umebakia tukipata viwanda au wawekezaji tunaweza kufikia," alisema.

Kwa upande wao wananchi wa visiwa hivyo wameishukuru serikali kwa kuwapatia huduma hiyo ndani ya visiwa vyao.

Asha Juma, miongoni mwa wakazi wa visiwa hivyo, alisema kuwapo kwa nishati hiyo kutabadilisha maisha yao kwa sababu shughuli zao kubwa ni uvuvi na watautumia kuhifadhi samaki na kuuza.

# Watoto watakiwa kujiepusha matumizi simu mkononi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WATOTO wametakiwa kuacha kutumia simu za mkono ili kuepuka kuangalia mambo mabaya ambayo yanaweza kusababisha kuingia katika vitendo vya udhalilishaji.

Meneja miradi kutoka Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, Ali Mohammed, aliyasema hayo wakati wa kuadhimisha Siku ya Mtoto wa Afrika, hafla iliyofanyika mjini Unguja.

Alisema watoto wanatumia simu za wazazi wao, na wengine kusajili kwa kificho hali inayohatarisha usalama wao hasa kwa vitendo vya udhalilishaji.

Mwenyekiti kutoka Muungano wa Asasi za kiraia Zanzibar, Asha Aboud, alisema wazazi wanajukumu kubwa la kuwalinda watoto ili kuwaepusha na matukio mbalimbali ya udhalilishaji.

Aliitaka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuangalia sera na sheria ili kuwapa fursa watoto wote kushiriki kikamilifu kupata haki zao za msingi ikiwamo elimu.

Alisema licha ya serikali kuimarisha miundombinu ya elimu, bado baadhi ya sera na sheria ni kandamizi kwa baadhi ya watoto hususani wenye ulemavu.

Alisema wakati umefika wa wazazi kuzingatia na kufuatilia mienendo ya watoto wao hasa kwa kuwaepusha kutumia simu.

Akiwasilisha ripoti ya utafiti wa ongezeko la vijana na watoto wa kiume kujihusisha na vitendo vya udhalilishaji, uliofanywa na TAMWA, mshauri muelekezi wa utafiti wa kihabari, Asha Abdi alisema, suala la utandawazi limeonekana ndiyo tatizo kubwa na kuonekana kwa kiasi kikubwa kuchangia vitendo vya udhalilishaji.

Alisema ripoti hiyo imebainisha vitendo hivyo siku hizi vimeongezeka kutokana na kuwapo uhamasishaji mkubwa wa kushajihishwa jamii kuripoti matukio hayo tofauti na miaka ya nyuma.

Akisoma risala kwa niaba ya watoto wenzake, Mwanafunzi Haitham Hussein, kutoka Shule ya Fujoni, aliiomba serikali na wadau kuandaa mipango thabiti ya kuwasaidia kupata malezi bora na ulinzi ili waweze kuepukana na vitendo vya udhalilishaji.

Alisema watoto wanaathiriwa na changamoto mbalimbali, kuwapo kwa hali hiyo itasaidia kwa kiasi kikubwa kuishi kwa amani na kufikia malengo yao.




Waziri wa Kilimo, Maliasili, Umwagiliaji na Mifugo, Shamata Shaame Khamis, akimkabidhi baiskeli miongoni mwa viongozi wa vikundi vya kuweka na kukopa vya kilimo cha viungo, Halima Makame kutoka Shehia ya Kidoti Mkoa wa Kaskazini Unguja. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Othman ataka taifa kuzalisha wasomi bora

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Massoud Othman, amesema wakati umefika kwa taifa kuzalisha wasomi watakaosaidia kuifanya elimu kuchangia kwa kina ukuaji wa haraka uchumi na maendeleo nchini.

Aliyasema hayo katika kipindi cha televisheni cha mazungumzo ya asubuhi cha Clouds Media mjini Dar es Salaam, alipokuwa na mahojiano maalum na kituo hicho kuhusu mambo mbalimbali yanayohusu, siasa, uchumi na maendeleo ya Tanzania.

Alisema Tanzania sio nchi maskini kutokana na rasilimali nyingi na muhimu zilizoko, lakini kinachokosekana ni mipango bora ya kuzalisha wataalamu wenye elimu itakayosaidia ukuaji imara wa uchumi kama zilivyofanya nchi kadhaa ikiwamo Singapore, Malaysia na nyingine nyingi duniani.

Alisema nchi hizo zikiangaliwa hazina rasilimali za kutosha kama ilivyo Tanzania, lakini kutokana na jitihada zao na muono mkubwa wa maendeleo wa viongozi, kumechangia kupiga hatua kubwa na kuingia katika orodha ya nchi zenye uchumi mkubwa duniani.

Kadhalika, alisema wakati umefika kwa Tanzania kujitahidi kuwa na sera bora na mipango madhubuti itakayochangia kuwafanya wasomi wanaozalishwa kwenye vyuo mbalimbali nchini iwe ni chachu na kichocheo muhimu cha kukuza uchumi na maendeleo taifa.

Akizungumzia maridhiano na Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar, Othman alisema bado misingi imara ya kuwapo serikali inahitaji kujengwa na kinachohitajika ni kuhakikisha kunatengenezwa mfumo bora wa kuimarisha serikali hiyo na kuifanya kuwa yenye manufaa zaidi kwa wananchi na kukuza maendeleo nchini.

Alisema hatua ya kujenga misingi imara ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa pia itachangia kuondoa msingi mkuu wa matatizo ya kisiasa yanayojitokeza kila mara ambayo ni kukosekana haki na kutokuwapo nidhamu pamoja na uwajibikaji mbaya kwa viongozi wa ngazi mbalimbali.

Akizungumzia Muungano ulioko, alisema maoni na msimamo wa chama chake cha ACT-Wazalendo ni kuwapo serikali tatu ambao ndiyo mfumo bora utakaosaidia kuiendesha nchi katika kupatikana haki kwa pande mbili.

Aliwasihi Watanzania kuwa na muono zaidi kwenye masuala mbalimbali ikiwa ni kutoyachukulia masuala yanayohusu Muungano kwa mtazamo wa kisiasa zaidi na badala yake kutafakari kwa mtazamo wa kimaendeleo ya mfumo bora unaopaswa kuwapo.

Kadhalika, Othman alisema mfumo uliopo sasa unaifanya Zanzibar yenye uchumi mdogo kuliko Tanzania Bara kuwa na mfumo sawa wa kodi jambo ambalo linaifanya kukosa kujikwamua na matatizo ya kiuchumi.

Alitoa mfano wa Hong Kong, Makao na Taiwan kwamba zote ni nchi zilizo chini ya Jamhuri ya Watu wa China, lakini zina mifumo ya kodi ambayo ni tofauti na kuziwezesha nchi hizo kupata mapato makubwa zaidi jambo ambalo pia linawezekana kwa Zanzibar.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NAURA SPRING LIMITED** inatangaza kupotea kwa kadi yake ya gari yenye namba za usajili **T 991 BWB - TOYOTA NOAH.** Chassis namba **AZR600021519.** Engine namba **1AZ4065509.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/251230/2022**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**YA WILAYA YA NJOMBE**
**KITUO CHA NJOMBE MJINI**
**MKOA NJOMBE**
**USIMAMIZI WA MIRATHI NA 37/2022**
**MWAJABU SEKALINGA.............MAREHEMU**
**KENANY KENETH**
**MBEYELA................MSIMAMIZI**

**TAARIFA KWA WADAI**
**(KANUNI YA 9(1)YA NYONGEZA YA V YA SHERIA YA MAHAKIMU WA MAHAKAMA SURA YA II REJEO LA 2019)**

TAARIFA INATOLEWA HAPA KWA WOTE WANAODAI KUWA NA MADAI YANAYOHUSIANA NA MALI ZA MAREHEMU MTAJWA HAPO JUU MWAJABU SEKALINGA ALIYEFIA NYUMBANI KWAKE TAREHE 25 MWEZI NOVEMBA MWAKA 2012,NA MAHAKAMA KUNIPA BARUA YA USIMAMIZI WAS MIRATHI HIYO MIMI KENANY KENETH MBEYELA SIKU YA TAREHE 21 MWEZI JUNI MWAKA 2022,HAPA SASA WANATAKIWA KUNIPA MADAI YAO KWANGU KUPITIA SANDUKU LANGU LA BARUA 345 NJOMBE AU NAMBA 0710986238 AU KUNILETEA KWA BINAFSI,NDANI YA SIKU 14 KUANZIA TAREHE YA KUTANGAZWA TAARIFA HII AMBAPO MUDA WAKE UTAPOISHA NITAENDELEA KUKABIDHI MALI ZA MAREHEMU KWA WARITHI WANAOSTAHILI,NIKIZINGATIA MADAI AMBAYO NITAKUWA NIMEARIFIWA.

K. Mbeyela
..........................................
**KENANY KENETH MBEYELA**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**KIPESE BUPAMBA MBOGO** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T232BKS** AINA YA **RAVER 4J.** CHASISI NAMBA **SXA11-7138320**, ENGINE NAMBA **3S2628199.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **MAN/BAB/RB/194282/2022.**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA BABATI**
**MKOA WA MANYARA**
**ELIZABETH TLAGHAT TSEAM......MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**1.FIDELIS KIMERI**
**2. AXWESSO TLAGHATE .....WAJIBU MAOMBI**

**AXWESSO TLAGHATE POPOTE ULIPO.**

Fahamu kwamba mleta Maombi E**LIZABETH TLAGHAT TSEAM** ameleta Maombi **Na.48/2022** dhidi yenu.
Hivyo basi kama unakusudia kupinga maombi hayo unatakiwa kuleta majibu yako na uwepo Barazani wewe binafsi, wakili wenu au mwakilishi anayekubalika kisheria, Shauri limepangwa kutajwa tarehe **27/6/2022.** Endapo hautatekeleza hayo shauri litasikilizwa upande mmoja na hukumu kutolewa.
**Imetolewa na kutiwa Saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 10/6/2022.**

2022. THE DISTRICT LAND AND HOUSING TRIBUNAL
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) BABATI

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**
**IN THE DISTRICT COURT OF BIHARAMULO**
**AT BIHARAMULO**
**CIVIL CASE NO...1/2022**
**HAMUDI ABDI SULEIMAN &**
**ANOTHER............../PLAINTIFF**
**VERSUS**
**1.JOSEPH SAMSON BUNDALA &**
**................../DEFENDANT**
**2.FRESTER INVESTMENT COM.LTD**

**TO, JOSEPH SAMSON BUNDALA**
**C/O FRESTER INVESTMENT CO.LTD**
**KAHAMA**

**TAKE NOTICE** THAT THE ABOVE MENTION CASE HAS BEEN SET DOWN FOR MENTION/ ON THE ...14TH ...DAY OF...JULY...2022 AT 9:00AM O'CLOCK IN THE FORENOON IN A VIEW OF FIXING HEARING DATE.
GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT THIS 16TH...DAY OF...JUNE...2022

**RESIDENT MAGISTRATE**
**BIHARAMULO**

**RECEIVED BY ..................**
**ON.......................................**
**SERVED BY...KAMUGISHA..**

RESIDENT MAGISTRATE
BIHARAMULO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**CHINA RAILWAY JIANCHANG ENGINEERING CO (T)** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA MITSUBISHI FUSO YENYE NAMBA ZA USAJILI **T499 BMH**, YEYOTE ATAKAYEIOKOTA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI **POLISI TAARIFA DAR/CHA/RB/252461/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ELIAKIMU KAVAKULE JULIUS** ANATANGAZA KUPOTEA KWA CHETI CHA KIDATO CHA NNE CHENYE INDEX NAMBA **S0360-065** KILICHOTOLEWA NA BARAZA LA MITIHANI LA TAIFA KUPITIA KISHOJU SEKONDARI MWAKA **1990.** KWA YEYOTE ATAKAYEKIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. **TAARIFA YA POLISI: DSM/PHQ/RB/252499/2022.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA MWANZO BOMA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**MOROGORO**
**USIMAMIZI WA MIRATHI NA...... /2021**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: WINHARD ADAM MOSHA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA: MARY EPHATA METTA**

**TANGAZO**
(KANUNI YA 5(2)YA KANUNI ZA USIMAMIZI WA MIRATHI MAHAKAMA ZA MWANZO)

WATU WOTE WANAODAI KUWA NA UHUSIANO WOWOTE/MASLAHI YOYOTE NA MIRATHI YA MAREHEMU TAJWA HAPO JUU,WANAALIKWA KUJA NA KUHUDHURIA KATIKA SHAURI HILI ENDAPO WAKITAKA KUFANYA HIVYO MNAMO TAHEHE 08 MWEZI 07 MWAKA 2022 KABLA HUYO MWOMBAJI HAJATEULIWA KUWA MSIMAMIZI WA MIRATHI HIYO.

**ZINGATIA;**

- ENDAPO KUNA YOYOTE MWENYE WOSIA NA MAREHEMU ANAWEZA KUULETA MAHAKAMANI KUKAGULIWA.
- WOSIA YA NAREHEMU HUYO UPO MAHAKAMANI WAWEZA KUKAGULIWA.
- MAREHEMU HAKUACHA WOSIA
- FUTA ISIYOHUSIKA.

**IMETOLEWA TAREHE 22 MWEZI 06 MWAKA 2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**MAWAZO MATOGO** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA CHETI CHA KIDATO CHA NNE CHENYE INDEX NAMBA **S0386-0098** KILICHOTOLEWA NA BARAZA LA MITIHANI KUPITIA SHULE YA SECONDARI YA GEITA MWAKA **1994** ,YEYOTE ATAKAYEKIOKOTA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CCHA POLISI
**POLISI TAARIFA DAR/CHA/RB/251856/2022**

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie***

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Lugha chafu kikwazo wanawake migodini

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

LUGHA chafu, matusi na kejeli kwa wanawake katika maeneo ya uchimbaji wa madini imetajwa kuwa chanzo kikubwa cha kundi hilo kuwa na woga wa kujihusisha na shughuli za uchimbaji madini katika maeneo mbalimbali ya migodi midogo nchini.

Mlezi wa wachimbaji madini ya dhahabu wanawake, William Machimu, alibainisha hayo jana alipotembelewa na vyombo vya habari katika mgodi mdogo wa Mwine wilayani hapo.

Alisema kuwa awali wanawake wengi waliokuwa wakijihusisha na uchimbai wa madini, walikuwa wakifanyiwa fujo na wachimbaji wanaume ikiwa ni pamoja na kuzomewa na kuchaniwa nguo, hali ambayo iliwajengea woga kujihusisha na uchimbaji.

Machimu alisema sasa serikali imeleta usawa mkubwa wa kijinsia katika shughuli za uchimbaji, tofauti na awali ambapo kwa sasa wanawake wamekuwa mstari wa mbele katika kujihusisha na uchimbaji wa madini ya dhahabu kwa kiasi kikubwa, hali ambayo imesadia kuleta mabadiliko katika maisha yao.

Alisema kuwa katika mgodi huo wa Mwime, kuna wanawake ambao wanaendesa maisha yao kwa uchotaji wa maji, ufuaji wa nguo, upishi, uchimbaji na kuponda mawe yanayosadikiwa kuwa na madini, hivyo kunufaika na fursa hiyo ya kiuchumi.

Mchimbaji mdogo Ester Charles alisema wamekuwa wakidharauliwa na wachimbaji wanaume na kuonekana kama mkosi pale wanapoingia shimoni kuchimba na hivyo kulazimika kuajiri vijana wa kiume kuingia ndani na kuchimba, wao wakibaki juu kupokea mawe yanayosadikiwa kuwa na madini.

Alisema dosari nyingine ni uwapo wa watoto wadogo sehemu ya migodi ambao wanajihusisha na vitendo ambavyo viko kinyume cha maadili.

Mchimbaji mwingine, Vumilia Wambula, aliiomba serikali kuwawezesha kwa kuwapatia mikopo na vifaa vya uchimbaji wa madini, ili kumudu soko la ushindani katika sekta ya madini.

Mwenyekiti wa Wachimbaji Wadogo Mkoa wa Kimadini Kahama, Joseph Nalemi, alisema kuwa kwa kushirikiana na serikali, wametenga eneo la Nyamishiga lililoko Kata ya Lunguya, Halmashauri ya Msalala kwa ajili ya wachimbaji wanawake.

Alisema uchimbaji wa madini unahitaji kuwa na mitaji mikubwa ya kuendesha kazi hiyo, jambo ambalo linakuwa mtihani kwa wachimbaji wadogo wanawake.

# Mwalimu aliyejifungua pacha 4 kupewa huduma maalum

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

MKUU wa Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma, Julius Mtatiro, amemtaka Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru kuanza mchakato wa kumhamishia kwenye shule iliyoko Tunduru mjini Mwalimu Judith Sichalwe (29), ambaye amejifungua watoto wanne bila upasuaji katika Hospitali ya Misionari ya Mbesa wilayani hapo.

Mtatiro alitoa maelekezo hayo jana alipomtembelea mwalimu huyo katika Kijiji cha Mkapunda na kumpa hongera kwa jambo hilo lisilo la kawaida.

Alisema mwalimu huyo inabidi ahamishwe kutokana na kubainika kuishi mazingira magumu katika eneo la kijiji hicho ambacho kina Shule ya Msingi Mkapunda iliyoko Km 100 kutoka mjini Tunduru.

Mtatiro alisema ni wajibu wa serikali kumrahisishia maisha bora mwalimu huyo ambaye anaweza kukabiliwa na hatari ya kushindwa kumudu gharama za maisha kutokana na idadi hiyo ya watoto wachanga aliowapata kwa wakati mmoja.

Ofisa Tarafa ya Nalasi ambako mwalimu huyo anaishi, Salum Kijumu, aliishukuru Ofisi ya Mkuu wa Wilaya kwa kuratibu misaada mbalimbali, akiwaomba Watanzania wote watakaoguswa na kazi ya malezi ya pacha hao wanne, kumsaidia mwalimu huyo.

Alisema Mtanzania atakayeguswa na akahitaji kumsaidia Mwalimu Judith, awasiliane na mwalimu huyo moja kwa moja kupitia namba 0673103536.

Nipashe ilimtafuta na kuzungumza naye ambapo pamoja na mambo mengine, alimshukuru Mkuu wa Wilaya kwa maelekezo hayo, akisisitiza kuwa atamhakikishia usalama wa watoto wake.

Alibainisha kuwa awali maofisa tabibu walimweleza kuwa ujauzito wake ulikuwa wa watoto watatu lakini alipokwenda kujifungua, wakawa watoto wanne, wa kike wawili na kiume wawili.

Mwalimu huyo alisema alijifungua watoto hao Mei 27, mwaka huu, hivyo jana walikuwa wanatimiza mwezi mmoja na kwamba huo ulikuwa ni ujauzito wake wa pili kwake wa kwanza akijifungua mtoto mfu.




Kundi la wahisani 26 kutoka Uswiss wakiwa kwenye lango la Mweka muda mfupi baada ya kushuka katika kilele cha Mlima Kilimanjaro ikiwa ni sehemu ya kutimiza azma yao ya kuchangisha fedha kwa ajili ya kusaidia wanawake na watoto Tanzania wenye mahitaji hasa wanaotoka kwenye familia maskini. **PICHA: ASIRAJI MVUNGI**

# Kampuni 180 za nje kushiriki maonyesho Sabasaba

**Na Grace Gurisha**

MKURUGENZI Mkuu wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (Tan Trade), Latifa Khamis, amesema kampuni 180 za nchi za nje na nchi 22 zitashiriki katika Maonyesho ya 46 ya Kimataifa ya Biashara (Sabasaba) mwaka huu na za ndani 3,200.

Khamis alisema hayo jana wakati akifungua semina kwa ajili ya washiriki wa maonyesho ya DITF kwa lengo la washiriki kufuata sheria na taratibu za maonyesho hayo.

Alisema kushiriki kwa kampuni hizo ni mafanikio makubwa, idadi hiyo ilikuja kwa bahati, lakini ni kazi kubwa iliyofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan katika diplomasia ya uchumi ambayo iliwasaidia kutotumia nguvu kuwaalika.

Alisema maonyesho ya Sabasaba yanatambuliwa na umoja wa taasisi zinazoandaa ulimwenguni ambalo ni Shirikisho Ufi, kwa sasa Tan Trade wanachama wa shirikisho hilo jambo ambalo nchi nyingi zilipata mwamko wa kushiriki kwa sababu hiyo.

Pia, alisema kwenye maonyesho hayo kutakuwa na kongamano kubwa la biashara Julai 5, 2022 litakalofanyika ukumbi wa Mwalimu Nyerere, wafanyabiashara watatakiwa wajitokeze kwa wingi kutokana na kuwapo kwa fursa za uwekezaji. Alisema pia kutakuwa na wanafunzi wa shule za msingi na sekondari kutoka Wilaya ya Babati, Bahi, Luhambwa, Kaskazini Unguja na wenyeji Dar es Salaam kwa ajili ya kufahamu maonyesho na kutambua maendeleo ya nchi.

Pia, alisema Julai Mosi kutakuwa na siku maalum ya Iran, Kituo cha Utamaduni kitaonyesha tamaduni zao katika viwanja vya Sabasaba ili Watanzania wafahamu fursa zilizoko Iran na Wairan wajue fursa zilizoko Tanzania.

Mtoa mada kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Temeke, Abdallah Seif Abdallah, aliwaomba washiriki hao kutoa risiti kwa wateja wao waepuke kulipa faini, kutokana na kuwa na wakaguzi risiti hizo kwenye mageti ya kutokea uwanjani.

Kwa upande wake, Masha Hussein kutoka Tan Trade, aliwaeleza washiriki hao mambo ambayo hayaruhusiwi kufanywa ndani ya viwanja hivyo ikiwamo silaha na mambo ya kivita na kila mshiriki anatakiwa kufuata sheria na taratibu zilizowekwa.

# MBEYA CITY YAFUNGUKA ILIPOWAKAMATA VIGOGO

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Mbeya City, Mathias Lule amefichua siri kubwa ya kuvuna pointi tano kutoka kwa Simba na Yanga kwenye mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu unaotarajiwa kufikia tamati kesho katika viwanja nane nchini.

Mbeya City ilifanikiwa kuifunga Simba katika mchezo wa mzunguko wa kwanza wakiwa nyumbani kwao jijini Mbeya na kukubali kupoteza ugenini na kuvuna pointi mbili dhidi ya Yanga, wakitoka nao sare ugenini na nyumbani.

Akizungumza na gazeti hili jana, Lule alisema licha ya kutofikia malengo yao ya kumaliza kwenye nafasi ya nne za juu katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara lakini wachezaji wake wamefanya kazi na kutoa mchango mkubwa msimu huu.

**Lule alisema anajivunia zaidi kikosi chake kwa sababu wachezaji wame pambana mbele ya vigogo hao na kufanikiwa kuvuna pointi tano kati ya alama 12 kutoka kwa mabingwa wapya wa ligi hiyo, Yanga na Simba ili yomaliza kwenye nafasi ya pili.**

"Niwapongeze vijana wangu kwa sababu wamefanikiwa kwa asilimia kubwa hasa kuvunja pointi tano kutoka kwa hizo klabu za Simba na Yanga, zimekuwa imara katika idara, lakini vijana wangu wamefanikiwa kufuata kile nilichowapa mazoezi na kufanya vizuri katika mechi tulizokutana nao," alisema Lule.

Alisema mechi hizo hazikuwa ngumu walipokutana na hizo timu kongwe kwa sababu alifanikiwa kutumia ubora wao ili kuvuta pointi.

Kocha huyo alisema ligi imekuwa ngumu na ushindani mkubwa kwa msimu huu na kuhakikisha wanaenda kujipanga kivingine kwa msimu ujao wa ligi hiyo.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Mbeya City yenye pointi 36, iko kwenye nafasi ya tisa wakati ndugu zao, Mbeya Kwanza iliyopanda daraja msimu uliopita imeshashuka daraka huku Prisons ikiwa kwenye hali tete.

Mbeya City itacheza mechi ya mwisho ya msimu huu nyumbani kwenye Uwanja wa CCM Kumbukumbu ya Sokoine dhidi ya Namungo FC kutoka mkoani Lindi.

Prisons yenyewe itafunga pazia la Ligi Kuu Tanzania Bara ugenini kwenye Uwanja wa Mabatini kwa kuwakabili Ruvu Shooting.




Mratibu wa mashindano ya Ndondo Cup, Yahya Mohamed (katikati), akizungumza wakati wa uzinduzi wa michuano hiyo itakayofanyika kwa mara ya kwanza katika mji wa Kahama. Kulia ni Katibu Mkuu wa Chama cha Soka Mkoa wa Shinyanga (SHIREFA), Michael Kaijage na Mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya chama hicho, Julius Lugobi. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Ndondo Cup 2022 yahamia Kahama

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

TIMU itakayofanikiwa kutwaa ubingwa wa mashindano Ndondo Cup yatakayofanyika kwa mara ya kwanza mjini hapo mwaka huu itajinyakulia zawadi ya Sh. milioni tano, imeelezwa.

Mratibu wa mashindano hayo, Yahya Mohamed, alisema usajili wa michuano hiyo itashirikisha timu 16 ulianza rasmi jana na kauli mbiu ni "Twende Pamoja" inayokwenda sambamba na uhamasishaji wa zoezi la sensa na chanjo ya Uviko-19.

Alisema kila timu itakayojiandikisha itatakiwa kulipa ada ya sh. 200,000 kwa ajili ya usajili lakini itapata vifaa vya michezo ikiwamo jezi na wanaahidi hakutakuwa na upendeleo kwa klabu yoyote.

Alitaja zawadi ya mshindi wa pili ni Sh. milioni tatu, timu zilizoingia hatua ya nusu fainali zitapata Sh. milioni moja kila moja huku kikundi kitachoongoza kwa uhamasishaji wakati wa michuano hiyo kitapata shilingi milioni moja.

Naye Katibu Mkuu wa Chama cha Soka Mkoa wa Shinyanga (SHIREFA), Michael Kaijage aliwapongeza waandaaji wa michuano hiyo kwa kukubali maombi yao ya kuanzisha Ndondo Cup kwenye mkoa huo kwa sababu itatoa nafasi ya kuibua vijana wapya wenye vipaji.

## Coastal Union yasaka heshima

**Na Cheji Bakari,** TANGA

BAADA ya kupoteza mchezo dhidi ya Kagera Sugar, Coastal Union imejipanga kuhakikisha inapata ushindi katika mechi yake ya mwisho ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Geita Gold FC itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini hapo.

Coastal Union iliruhusu kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa Kagera Sugar na kutibua mipango ya timu hiyo kumaliza ligi hiyo katika nafasi nne za juu.

Katika msimamo wa ligi hiyo, Coastal Union iko kwenye nafasi ya saba ikiwa na pointi 37 wakati Kagera Sugar ilipaa hadi nafasi ya sita ikiwa na alama 38.

Akizungumza na gazeti hili jijini hapo jana baada ya mazoezi ya asubuhi yaliyofanyika kwenye viwanja vya Popatilal, Kocha Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda alisema ameyafanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza ili kuhakikisha wanamaliza msimu kwa heshima.

Mgunda alisema pia amefanya kikao na wachezaji wake kwa ajili ya kuhakikisha hawarudii makosa yaliyofanyika katika mechi iliyopita ili kuwapa furaha mashabiki wao kwa kuwaunga mkono wakati wote wa msimu huu unaotarajiwa kumalizika kesho.

"Nimetoka mazoezini na sasa nipo katika kikao na wachezaji wangu ili kupeana mawili matatu kuelekea mechi dhidi ya Geita Gold FC, tunataka kumaliza kwa heshima," alisema Mgunda.

Naye Msemaji wa Coastal Union, Miraji Wandi alisema katika mechi iliyopita kikosi cha Coastal Union kilionyesha uwezo mkubwa lakini wapinzani wao Kagera Sugar walitumia vyema nafasi waliyoipata na kuibuka na ushindi.

## Geita yajipanga kumlipa Ndayiragije

**Na Adam Fungamwango**

UONGOZI wa Geita Gold FC inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara imeahidi kumlipa aliyekuwa Kocha Mkuu wa timu hiyo, Etienne Ndayiragije kwa sababu jambo hilo limo ndani ya uwezo wao.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Geita Gold, Simon Shija, alisema klabu hiyo imepokea barua kutoka katika Shirikisho la Soka Duniani (FIFA) likitoa maelekezo hayo na wao wako tayari kuifanyia kazi haraka ili kukidhi matakwa na kuendelea na taratibu za usajili.

"Klabu imepokea maelekezo na kwa sababu ni mambo ya kisheria inafanyia kazi kwa haraka ili kukidhi matakwa na kuendelea na taratibu za usajili. Uongozi unatambua umuhimu wa jambo hili na tunawasihi mashabiki, wapenzi na wadau wetu watulie, jambo hili lipo ndani ya uwezo wa klabu," alisema kiongozi huyo.

Mwishoni mwa wiki, Shirikisho la Soka Nchini (TFF) lilitoa taarifa inayotoka FIFA ya kuifungia timu hiyo kusajili kwa miaka miwili mpaka pale itakapomlipa kocha huyo raia wa Burundi.

Geita Gold iliachana na kocha huyo tangu Oktoba mwaka jana akiwa ameiongoza katika michezo minne tu.

## ZISIKUPITE

### JESUS, CITY KIMEELEWEKA

MSHAMBULIAJI wa Manchester City na Timu ya Taifa ya Brazil, Gabriel Jesus mwenye umri wa miaka 25, amekubali mkataba wa miaka mitano na Arsenal. ***(Guardian)***

### BELLINGHAM MAMBO SAFI

LIVERPOOL wana uhakika wa kumsajili kiungo wa kati wa Borussia Dortmund na Timu ya Taifa ya England, Jude Bellingham. ***(Sun)***

### WARD-PROWSE KUTUA WEST

KLABU ya West Ham ina nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Southampton na Timu ya Taifa ya England, James Ward-Prowse mwenye umri wa miaka 27, msimu huu wa joto. ***(Sky Sports)***

### ERIKSEN AGOMBEWA SOKONI

NYOTA wa Denmark, Christian Eriksen anakaribia kufanya uamuzi kuhusu mustakabali wake, huku Tottenham Hotspur sasa wakionyesha nia lakini Brentford wana matumaini ya kumnunua tena mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30. ***(Fabrizio Romano)***

### WAKALA WA MANE AFUNGUKA

WAKALA wa Sadio Mane amekanusha taarifa kuwa fowadi huyo wa Senegal mwenye umri wa miaka 30, aliondoka Liverpool na kujiunga na Bayern Munich msimu huu wa joto kwa sababu alikuwa akilipwa mshahara mdogo. ***(TVMondo, via Mirror)***

### WEST, VILLARREAL ZATETA

KLABU za Villarreal na West Ham zimefanya mazungumzo juu ya mauzo ya winga wa Timu ya Taifa ya Uholanzi, Arnaut Danjuma mwenye umri wa miaka 25. ***(Toni Juanmarti)***

### UNITED YATENGA KITITA

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag anaweza kuwa na pauni milioni 100 tu kuijenga upya klabu hiyo msimu huu wa joto. ***(Sun)***

### SPURS YAMFUATA JOSKO

KLABU ya Tottenham Hotspur imemuulizia beki wa RB Leipzig na Timu ya Taifa ya Croatia, Josko Gvardiol mwenye umri wa miaka 20. ***(Nabil Djellit)***

### DI MARIA KUTUA JUVE

ANGEL di Maria mwenye umri wa miaka 34, ambaye mkataba wake na Paris St-Germain unamalizika mwishoni mwa Juni, anakaribia kuhamia Juventus. ***(Calciomercato)***


### WILLIAMS NJIA MOJA

MLINZI wa Manchester United, Brandon Williams mwenye umri wa miaka 21, hana mahitaji ya ziada Old Trafford na anaweza kupatikana kwa pauni milioni 10 msimu huu wa joto. ***(Mail)***

### JURANOVIC AWINDWA

KLABU ya Atletico Madrid inamfuatilia beki wa Celtic na Timu ya Taifa ya Croatia, Josip Juranovic mwenye umri wa miaka 26. ***(Record)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# UNITED YAKARIBIA KUMSAJILI DE JONG

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United inakaribia kufikia mwafaka na Barcelona kuhusu kumnunua kiungo wa kati, Frenkie de Jong, kwa mujibu wa 90min.

**United ilikataliwa ofa ya kwanza ya takribani euro milioni 65 ili kumsajili raia huyo wa Uholanzi mwenye umri wa miaka 25, lakini sasa wapo kwenye nafasi nzuri ya kukamilisha usajili huo.**

Hiyo ni baada ya kocha wao mpya, Erik ten Hag kutaka kuungana na mchezaji huyo ambaye aliwahi kumnoa alipokuwa Ajax.

**●●● Uamuzi huo utamfurahisha kocha wa zamani wa kiungo huyo ambaye...**

Barcelona wanataka dau la euro milioni 85 na vyanzo vimethibitishia 90min kwamba, United wameboresha ofa yao hadi euro milioni 80.

Inafahamika Barcelona bado wanaisukuma United kupanda juu zaidi, ingawa Mashetani Wekundu hao wanasita kufikia bei hiyo huku wakijiandaa kumlipa mshahara mkubwa pia.

United wamemfahamisha Ten Hag kuhusiana na dili la kumnunua De Jong liko karibu, huku bosi huyo akitamani kuungana tena na nyota wake wa zamani wa Ajax ili kuanza ujenzi wake Old Trafford.

Mahitaji ya kibinafsi ya De Jong tayari yamejadiliwa kati ya United na wawakilishi wake mapema mwezi huu na hayaonekani kama suala kubwa, huku akitarajiwa kuwa mmoja wa wachezaji wanaolipwa fedha nyingi zaidi klabuni hapo, nyuma ya Cristiano Ronaldo na David De Gea.

Viongozi wa United wana matumaini ya kukamilisha dili la kumnunua De Jong katika wiki ijayo na kuanza kwa maandalizi ya msimu mpya.


LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 267,

MECHI KALI
ZAMALEK
VERSUS
CERAMICA CLEOPATRA
1 | 1.76
X | 3.41
2 | 4.71

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# WAKALA AKANUSHA MANE KULIPWA KIDOGO LIVER




**MUNICH,** Ujerumani

MWAKILISHI wa Sadio Mane amesisitiza mchezaji huyo hakutaka kuondoka Liverpool kwa sababu alikuwa akilipwa mshahara mdogo.

Mane alijiunga na Liverpool mwaka wa 2016 na kusaini mkataba mpya mapema msimu wa 2018/19, ambao ulikuwa siku za mwanzo za kupanda kwake nyota, na ilisemekana alikuwa akipokea mshahara wa pauni 100,000 kwa wiki pale Anfield.

Imesemekana Mane alihisi kutoheshimiwa na Liverpool na hivyo kulazimika kuondoka klabuni hapo, lakini wawakilishi wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Senegal wamepuuza uvumi huo.

"Huo ni uvumi wa uongo," alisema wakala Bacary Cisse akiimbia TV5Monde.

"Mchezaji wa kiwango cha Sadio hawezi kupata mshahara ambao watu wanazungumza. Namba zinazozunguka sio sahihi kabisa.

"Sadio alikuwa tayari analipwa zaidi ya hapo alipojiunga na Liverpool kutoka Southampton. Aliongeza mkataba wake mwaka 2018 na mshahara wake ulikuwa mkubwa zaidi kuliko namba zinazosambazwa kwenye vyombo vya habari."

Mane anaaminika kuondoka Liverpool kutafuta changamoto mpya, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 akifahamu ana muda mdogo uliosalia kucheza katika kiwango cha juu.



## *Bayern yakomaa na Lewandowski*

**MUNICH,** Ujerumani

BAYERN Munich wanataka angalau pauni milioni 60 ili kumuuza, Robert Lewandowski kwa Barcelona.

Mapema wiki hii, Barcelona walitoa ofa ya pauni milioni 34.4, lakini Bayern walisisitiza mshambuliaji huyo hauzwi, ingawa amebakiza mwaka mmoja tu kwenye mkataba wake.

Mwezi uliopita, Sky Germany iliripoti mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 aliiambia Bayern hataongeza mkataba wake hadi mwisho wa msimu wa 2022/23.

Lewandowski ameiambia klabu hiyo ya Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, anataka kupata changamoto mpya.

Sky iliongeza Lewandowski angependa kuhamia Barcelona msimu huu wa joto badala ya kusubiri kuwa mchezaji huru.

Oliver Kahn, Mtendaji Mkuu wa Bayern Munich, aliiambia Amazon Prime, Aprili mwaka huu kuwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Poland hataondoka Allianz Arena msimu huu wa joto.

Lewandowski amekuwa na mabingwa hao wa Ujerumani tangu mwaka 2014 na ameifungia klabu hiyo mabao 344 katika michuano yote.

,714,020

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 28/06/22 | 20:00 | Ghazl EL Mahallah vs Ismaily SC | 3.11 | 2.76 | 2.56 |
| 02. 28/06/22 | 20:00 | Arab Contractors vs National Bank | 2.66 | 2.96 | 2.76 |
| 03. 29/06/22 | 01:00 | Brusque SC vs Bahia BA | 2.79 | 2.94 | 2.50 |
| 04. 29/06/22 | 03:30 | Corinthians vs Boca Juniors | 2.17 | 2.95 | 3.34 |
| 05. 29/06/22 | 13:00 | Daegu vs Pohang Steelers | 2.38 | 3.24 | 2.70 |
| 06. 30/06/22 | 01:00 | Nautico PE vs Criciuma SC | 2.47 | 3.12 | 2.67 |
| 07. 30/06/22 | 01:15 | Talleres vs Colon Santa Fe | 2.26 | 2.95 | 3.14 |
| 08. 30/06/22 | 02:00 | Orlando City vs Nashville SC | 2.32 | 3.15 | 2.85 |
| 09. 30/06/22 | 02:30 | Toronto FC vs Columbus Crew | 2.61 | 3.68 | 2.47 |
| 10. 30/06/22 | 03:00 | Chicago Fire vs Philadelphia Union | 2.47 | 3.27 | 2.86 |
| 11. 30/06/22 | 03:05 | Tlaxcala FC vs Cimarrones De Sonora | 2.41 | 3.10 | 2.76 |
| 12. 30/06/22 | 03:30 | CRB AL vs Tombense MG | 2.27 | 2.94 | 3.13 |
| 13. 30/06/22 | 03:30 | Novorizontino SP vs Vasco da Gama | 2.85 | 2.85 | 2.51 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 28/06/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 2601 | Shandong Luneng vs Henan Jianye | 2.06 | 3.23 | 3.28 |
| 14:30 | 4271 | Guangzhou RF vs Dalian Aerbing | 3.79 | 3.39 | 1.85 |
| 15:00 | 1286 | Mjondalen 2 vs Tromso IL 2 | 1.60 | 4.63 | 3.84 |
| 15:00 | 3609 | Rubin Kazan vs Kryliya Sovetov | 3.45 | 3.30 | 2.05 |
| 15:00 | 5658 | SV Darmstadt vs SV Elversberg | 1.28 | 5.51 | 7.28 |
| 16:00 | 1446 | Johor Darul Takzim vs FC Petaling Jaya City | 1.13 | 6.70 | 14.77 |
| 16:00 | 3030 | Selangor FC vs Sabah | 1.71 | 3.53 | 4.32 |
| 16:00 | 5269 | Adama City FC vs Dire Dawa Kenema FC | 2.35 | 2.66 | 3.35 |
| 17:00 | 3207 | BSC Young Boys vs Neuchatel Xamax | 1.23 | 6.09 | 8.25 |
| 18:00 | 1108 | Moldova W vs Lithuania W | 4.23 | 3.93 | 1.64 |
| 18:00 | 1319 | Kuressaare vs Levadia Tallinn | 11.78 | 6.28 | 1.17 |
| 18:00 | 2719 | Slovakia U19 vs Austria U19 | 2.74 | 3.33 | 2.30 |
| 18:00 | 3091 | Kokand 1912 vs Dinamo Samarqand | 1.63 | 3.64 | 4.72 |
| 18:00 | 3617 | England U19 vs Italy U19 | 1.86 | 3.53 | 3.58 |
| 18:30 | 3861 | FC Honka/Akatemia vs Musa Pori | 1.91 | 3.74 | 3.25 |
| 18:30 | 5599 | Lahti vs Japs | 1.19 | 6.30 | 9.84 |
| 19:00 | 2070 | Kaapo Kaarina vs Tampere United | 4.73 | 4.44 | 1.51 |
| 19:00 | 2243 | Estonia W vs Kazakhstan W | 3.80 | 3.90 | 1.79 |
| 19:30 | 1694 | Sweden W vs Brazil W | 2.03 | 3.34 | 3.24 |
| 20:00 | 1107 | Arab Contractors vs National Bank | 2.66 | 2.96 | 2.76 |
| 20:00 | 1984 | Halmstads BK vs Trelleborgs FF | 1.66 | 3.97 | 4.88 |
| 20:00 | 2137 | New Zealand W vs Wales W | 2.51 | 3.39 | 2.46 |
| 20:00 | 2315 | Norrby IF vs Ostersunds | 1.44 | 4.48 | 6.92 |
| 20:00 | 3408 | Grorud IL 2 vs Skeid Fotball 2 | 2.46 | 4.33 | 2.16 |
| 20:00 | 3857 | Ghazl EL Mahallah vs Ismaily SC | 3.15 | 2.80 | 2.49 |
| 20:00 | 4103 | IFK Lidingo vs FC Stockholm Internazionale | 9.40 | 5.29 | 1.24 |
| 20:00 | 5040 | Jonkopings Sodra vs Orgryte IS | 2.47 | 3.51 | 2.70 |
| 20:00 | 5408 | Tallinna Kalev vs Nomme Kalju | 9.40 | 5.68 | 1.22 |
| 20:30 | 2021 | Lindome Gif vs Gais | 5.09 | 4.41 | 1.48 |
| 21:00 | 3948 | France U19 vs Israel U19 | 1.32 | 4.91 | 7.07 |
| 21:00 | 4489 | Belgium W vs Luxembourg W | 1.01 | 16.73 | 29.52 |
| 21:30 | 3118 | B71 Sandoy vs KI Klaksvik II | 2.23 | 4.22 | 2.41 |
| 22:15 | 5345 | Augnablik W vs Haukar W | 2.99 | 3.73 | 2.01 |
| 22:30 | 2531 | Zamalek vs Ceramica Cleopatra | 1.76 | 3.41 | 4.71 |

JUMATANO - 29/06/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01:00 | 2295 | Brusque SC vs Bahia BA | 2.71 | 3.00 | 2.51 |
| 01:00 | 3130 | Gremio vs Londrina PR | 1.41 | 3.93 | 7.26 |
| 01:15 | 4242 | SC Emelec vs Atletico Mineiro | 4.11 | 3.42 | 1.77 |
| 01:15 | 5629 | Nacional (URU) vs Union Santa Fe | 2.13 | 3.10 | 3.25 |
| 02:00 | 5749 | USA U20 vs Costa Rica U20 | 1.34 | 4.72 | 7.09 |
| 02:00 | 5914 | Hartford Athletic vs Colorado Springs | 3.10 | 3.83 | 1.94 |
| 03:30 | 2482 | Guarani SP vs Ituano SP | 2.20 | 2.94 | 3.28 |
| 03:30 | 3555 | Vila Nova GO vs Ponte Preta | 2.11 | 2.91 | 3.55 |
| 03:30 | 4131 | Corinthians vs Boca Juniors | 2.17 | 2.95 | 3.34 |
| 03:30 | 4400 | Colo Colo vs Internacional | 2.03 | 3.24 | 3.34 |
| 03:30 | 4635 | Cruzeiro vs Sport Recife | 1.64 | 3.19 | 5.69 |
| 03:30 | 5868 | Atletico Pr vs Libertad Asuncion | 1.75 | 3.30 | 4.43 |
| 04:00 | 5510 | San Antonio vs Tulsa Roughnecks | 1.62 | 3.88 | 4.42 |
| 05:00 | 2227 | Panama U20 vs Honduras U20 | 3.87 | 3.77 | 1.73 |
| 10:30 | 1348 | Shanghai SIPG vs Shanghai Shenhua | 2.17 | 3.10 | 3.15 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# MWENDWA ASAINI SIMBA, ATAMBA MATAJI YATAREJEA

**Na Saada Akida**

KATIKA kuhakikisha mambo hayaharibiki, hali ya usiri imetawala katika mchakato wa usajili wa wachezaji wapya wa Simba ambapo tayari wamefanikisha usajili wa winga wa kimataifa kutoka Kenya, Harrison Mwendwa anayetokea Kabwe Warriors ya Zambia.

**Mwendwa alikuwa nchini na tayari juzi amerejea kwao baada ya kukamilisha ofa yake ya kujiunga na Simba kwa kusaini mkataba wa miaka miwili.**

Akizungumza na gazeti hili kabla ya kuondoka nchini, Mwendwa alisema akiwa jijini amefanya mazungumzo na timu tatu lakini amefanikiwa kusaini na klabu ambayo walikamilisha makubaliano vyema.

"Nilikuwa na mazungumzo na timu tatu lakini moja (bila kutaja jina) imefanikiwa ila kwa sasa ni mapema sana siwezi kuweka wazi ni timu ipi ila muda ukifika kila kitu kitakuwa wazi," alisema winga huyo.

Taarifa kutoka Simba zinasema winga huyo atarejea nchini kwa ajili ya kuanza maandalizi ya msimu mpya.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez, alikaririwa akisema wanaendelea vyema na usajili ingawa kwa sasa bado hawajaamua kuweka wazi nyota wengine waliowanasa ukimwondoa Moses Phiri ambaye walishamtambulisha.

"Mashabiki wanatakiwa kutulia kwa sababu mchakato wa usajili unaendelea, tayari kuna wachezaji tumewasajili, hatutafanya mabadiliko makubwa katika kikosi chetu, tumeleta vifaa kulingana na mahitaji ya timu na tumeshirikiana vizuri na kocha wetu mpya ambaye tutaratajia kuwa naye," alisema Barbara.

Simba imepoteza mataji yote matatu iliyokuwa inayashikilia na itamaliza msimu huu ikiwa katika nafasi ya pili kutokana na pointi walizonazo haziwezi kufikiwa na timu za chini yake kwenye msimamo wa ligi.

Wekundu hao wa Msimbazi watafunga pazia la Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2021/2022 ugenini kwa kuwavaa Mbeya Kwanza kwenye Uwanja wa Majimaji ulioko Songea, mkoani Ruvuma.




Askari wa Jeshi la Polisi akiwaongoza mashabiki wa Yanga waliojitokeza kuipokea timu yao baada ya kukabidhiwa kombe la ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2021/2022. Ligi hiyo inatarajiwa kumalizika kesho kwa timu zote 16 kushuka dimbani. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Askari afariki katika marathon*

**Na Rose Jacob,** MWANZA

ASKARI wa Jeshi la Magereza jijini Mwanza, Fidelis Mbigili (51), mwenye cheo cha Mrakibu Mwandamizi (SSP), amefariki dunia wakati akikimbia mbio za Lake Victoria Marathon, imeelezwa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Ramadhan Ng'anzi alisema tukio hilo lilitokea juzi na marehemu alikuwa akikimbia mbio za kilomita tano.

Ng'anzi alisema marehemu wakati akimalizia mbio hizo alianguka na kupoteza maisha katika makutano ya barabara ya Makongoro, Kenyata na Nyerere.

Naye Mkuu wa Jeshi la Magereza Mwanza, Lazaro William, alisema marehemu alishiriki mbio hizo akipewa namba 110 na mwili wake ulisafirishwa jana kuelekea kwao Iringa kwa ajili ya mazishi.

Baadhi ya washiriki wa mbio hizo ambao hawakutaka kutaja majina yao, walisema uratibu wa mbio hizo haukuwa mzuri kwa sababu wanariadha wote walitumia njia moja na hivyo baadhi walishindwa kutambua umbali waliostahili kushiriki.

Pia wameziomba mamlaka husika kuhakikisha washiriki wote wa mbio wanapimwa afya na kuacha tabia ya kuwapima wanariadha maarufu wanaojulikana.

# Michezo

Jumanne Juni 28, 2022

Nipashe




United yakaribia kumsajili de Jong UKURASA 21

# Siri Ubingwa Yanga SC hii

## ●●● Yajipanga kumtambulisha kisasa nyota Ki Aziz ambaye...

**Adam Fungamwango na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kusota miaka minne bila ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, hatimaye Kocha Mkuu wa Mbeya City, Mathas Lule amesema Yanga ilifanikiwa kutwaa taji hilo msimu huu kwa sababu ilikuwa na kiwango bora wakati wote.

**Yanga ilitwaa ubingwa wa msimu wa 2021/2022 ikiwa imebakisha mechi nne mkononi ikifuatiwa kwa tofauti ya pointi 10 na watani zao, Simba ambao walikuwa wanashikilia taji hilo kwa miaka minne mfululizo.**

Lule aliliambia gazeti hili mabingwa hao wapya walizizidi uwezo timu nyingine 15 zilizokuwa zinashiriki Ligi Kuu Tanzania Bara licha ya baadhi ya mechi kupata ushindi finyu.

Kocha huyo alisema kitimu Yanga haikuwa bora sana ila wachezaji wao wa nafasi ya viungo walikuwa bora kuliko timu nyingine na ndiyo chachu ya wao kutwaa ubingwa msimu huu.

Alisema unapocheza na Yanga msimu huu ilikuwa ni lazima uwasome, na kuwaelekeza wachezaji wako kuongeza umakini .

"Siyo ubingwa tu, tuseme tu ukweli Yanga ilichozizidi timu zote za Ligi Kuu msimu huu ni viungo. Wana viungo wenye ubora sana kwa hiyo ukitaka kucheza nao ni lazima uwasome, upange mikakati ya wachezaji kuitekeleza. Mfano mimi kwenye mechi yetu ya Jumamosi, Yanga walicheza mfumo wa 4-2-3-1.

Kwa hiyo nikapanga mikakati wa kuwazuia viungo wao, Jamal (Dulaz) aliondoka na Aucho (Khalid), Aziz (Andambwile) alikuwa anakaa na kiungo mmoja na Eliud (Ambukile) alikuwa anakaa na mmoja, hawa ukiwazuia kucheza basi unakuwa umeiua nguvu, kwa sababu ndiyo wanapiga mipira mirefu inayokwenda kwa mawinga na kuleta madhara. Ukiwaacha huru kucheza utaumia, ndiyo maana msimu huu hawakutufunga sisi," alisema Lule.

Ni Mbeya City na Simba tu ndiyo timu pekee ambazo Yanga imeshindwa kuzifunga kwenye Ligi Kuu, ikishindwa kupata pointi nne au sita, badala yake kugawana pointi moja moja.

Naye Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli amesema wanachama na mashabiki wameonekana kuwa na furaha isiyo kifani kwa sababu walipoteza ubingwa huo kwa misimu minne na tena muda wote taji lilikuwa linashikiliwa na watani zao wa jadi, Simba.

Wakati huo huo, Bumbuli alisema wanatarajia kumtambulisha mshambuliaji wao mpya wa kimataifa, Stephane Aziz Ki kutoka Asec Mimosas hapo kesho na usajili wake unatarajiwa kukiongezea nguvu kikosi chao kuelekea katika michuano ya kimataifa.

Kiongozi huyo alisema mshambuliaji huyo anatua nchini baada ya kumalizana naye ni mkataba wa miaka mingapi wameingia naye, wataweka hadharani siku ya utambulisho.

"Tunatarajia kumtambulisha Stephane Ki Aziz Jumatano, kama hamtamwona siku hiyo mtamwona siku zinazofuata, kila kitu kimekamilika na kinachotakiwa ni kuwa na subira," alisema Bumbuli.

Aliongeza Kocha Mkuu wa timu hiyo, Nasreddine Nabi amehitaji kupata nyota wapya watano ambao wanacheza nafasi za winga, mshambuliaji mchezeshaji, mfungaji wa haraka pamoja na mlinzi wa kushoto.

"Saido ameondoka hivyo lazima tufanye usajili wa mchezaji ambaye ataziba nafasi yake ili kuwa na kikosi kipana ambacho kitaleta ushindani kwenye michezo ya kimataifa pamoja na Ligi Kuu Tanzania Bara katika msimu ujao," Bumbuli aliongeza.

Kuhusu kutwaa ubingwa, alisema wametimiza kikamilifu malengo yao na wanawapongeza mashabiki wote wa klabu hiyo.

"Msimu haukuwa rahisi, tulikutana na changamoto mbalimbali ambazo zilikuwa zinatukatisha tamaa lakini tuliziba masikio ili tutimize jambo letu," alisema ofisa huyo.

Kwa upande wake Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Cedrick Kaze alisema amefurahi kupata ubingwa akiwa anaitumikia Yanga.

Kaze alisema msimu huu ulikuwa na ushindani kwa sababu timu zote zilijipanga vizuri ili kujinusuru na janga la kushuka daraja.

"Katika miaka 15 yangu ya mpira sijawahi kukutana na mapokezi makubwa kama haya niliyoyaona leo ninawashukuru mashabiki wetu kwa mapokezi mazuri, tumeona jiji limezizima," Kaze alisema.



Mwenyekiti wa Yanga, Dk. Mshindo Msolla (kushoto), akiwa amelishikilia kombe la ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2021/2022 ambao unamalizika kesho. Kulia ni nahodha wa timu hiyo, Bakari Mwamnyeto. **PICHA: MTANDAO**

## Simba yamchambua Sakho

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imesema kwa sasa haina ofa kutoka kwa timu yoyote ikieleza inamhitaji kiungo mshambuliaji wake, Pape Sakho, baada ya ofa ya awali kutoka Al Hilal ya Sudan kushindikana.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, aliliambia gazeti hili jana ofa kutoka Al Hilal ya Sudan ilikuwa nzuri, lakini muda walioiwasilisha wakati huo haukuwa rafiki kumuuza mchezaji huyo raia wa Senegal.

"Kwa sasa hakuna ofa yoyote iliyokuja kumtaka Sakho, tuliweka wazi huko nyuma kuwa ilikuja ofa kutoka Sudan na ilikuwa nzuri tu, lakini muda haukuwa rafiki kufanya hiyo biashara, ikashindikana," alisema Ahmed.

Aliongeza falsafa ya Simba miaka yote ni pamoja na kucheza soka na kununua wachezaji, lakini inafanya biashara ya mpira ambayo ni kuuza wachezaji na kutafuta wengine mbadala wake.

"Mchezaji mzuri lazima azungumzwe kuuzwa, huwezi kuwa na wachezaji kama umewazaa wewe, wala hawahusishwi na timu yoyote, lakini Sakho anatajwa huku na huko kwa sababu ya kiwango chake na sisi tunafurahi kuona wachezaji wetu wanahusishwa na klabu mbalimbali Afrika, hata sasa ikija ofa nzuri tutaiangalia, kwa sasa bado yupo sana Simba," Ahmed alisema.

Kiungo huyo mshambuliaji alisajiliwa Simba akitokea Teungueth ya Senegal na licha ya timu kutokuwa na msimu mzuri, nyota huyo amekuwa msaada mkubwa kwa kuiwezesha kufika hatua ya robo fainali ya michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >